ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Moja - Tarehe 26 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mgeni Hassan Juma) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/14 -

Wizara ya Mifugo na Uvuvi

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kwanza sina budi kutoa shukurani zangu na kumpongeza Waziri wa Mifugo kwa kazi nzuri sana waliyoifanya katika kuleta hotuba hii, na tumeweza kuijadili kwa Wajumbe wengi. Vile vile nichukue nafasi hii kuwashukuru Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyokuwa wameifanya.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikitaka nianzie kwa kusema kwamba Waziri wa Mifugo, Mhe. Jihad, na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Mhe. Maalim Haroun, shughuli zao ukizitazama zimefanana sana, kwa sababu lengo lao ni moja, shughuli zao ni moja, lengo na madhumuni ni kutaka kupunguza umasikini wa kipato kwa vijana wa kike na wa kiume, na vile vile kuweza kukuza ajira na vile vile kuongeza kipato cha taifa.

Mhe. Mwenyekiti, Mawaziri hawa wawili ni muhimu sana katika kuwasaidia wananchi kwa sababu shughuli zao ni za kuleta maendeleo na kuweka ajira kwa wananchi, kwa hiyo hii ni kama *triangle* baina ya Waziri wa Mifugo pamoja na Waziri wa Kazi, Uwezeshaji wakishirikiana pamoja na Waziri wa Fedha, watu watatu hawa wanafanya kama kitu cha *triangle*, yaani ni watu ambao wanahitaji kuwa pamoja katika kushirikiana kuandaa shughuli zao kwa pamoja na kuangalia namna gani wanaweza kuwasaidia wananchi ili na wao kujikomboa katika umasikini. Kwa hivyo hawa wote nia yao ni moja; ni katika kufanya Wizara hizi mbili muhimu na kulisukuma gurudumu hili ili wananchi wetu waweze kupata maendeleo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kuwa Waziri wa Fedha hivi sasa hayupo, katika hotuba hii ya Waziri, mgao wa fedha ni mdogo sana. Kwa hiyo hapa kama ingelikuwa Waziri wa Fedha yupo ilikuwa asikie maelezo haya kuona kwamba Wizara hizi mbili zinahitaji kuangaliwa sana, ili katika mgao huu wa fedha kwa wao uwe ni muhimu kwa sababu lengo na kazi zao zinafanana, na nia na madhumuni na ilani ya CCM inasema kuwasaidia wananchi kuwakomboa katika umasikini. Kwa hiyo hizi Wizara mbili zikishirikiana pamoja Mhe. Waziri wa Fedha hana budi kuwasaidia Wizara hizi mbili zikaweza kujikomboa. Kwa hivyo Mhe. Waziri, atafahamu baadae kwamba na yeye anahitajika kutoa msukumo wake na kuziangalia kwa jicho la huruma Wizara hizi mbili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze kwenye Wizara ya Mifugo, kutaka niseme tu kwamba katika Wizara ya Mifugo tunazo aina mbili za mifugo. Kuna mifugo ile ya asili na tunayo mifugo ya kisasa. Lengo la mifugo hii ni kuongeza uzalishaji na lengo la pili ni katika suala zima la kutaka kupunguza umasikini. Suala la upunguzaji umasikini kama nilivyozungumza linahitaji mashirikiano mazuri baina ya Wizara mbili hizi. Wananchi wetu hili suala la mifugo ya asili ni lazima tuangalie vizuri sana, kwa sababu shughuli zetu wananchi wa Zanzibar ni mifugo pamoja na uvuvi.

Kwa hivyo nilitaka nimwambie tu Mhe. Waziri, kwamba ni vyema hawa wafugaji wa asili, na kwa sababu shughuli zetu ni za asili ni lazima wapewe kipaumbele, wafugaji hawa wasipuuzwe, wafugaji hawa watembelewe, wafugaji hawa wanahitaji kuwaona madaktari wanatoa utibabu kwa wanyama wao na kuweza kutoa dawa ambazo ni muhimu kwa ajili ya mifugo yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuna suala zima katika Wizara zetu tunakosa kitu muhimu sana ambayo ni majosho, majosho kwa ajili ya kuogoshea ng'ombe wetu hayapo. Kwa hiyo Mhe. Waziri, mbali ya kutoa kipaumbele kwa wananchi wetu wafugaji lakini matibabu ni kitu muhimu kwa ajili ya wanyama wetu na kuweka katika afya nzuri na majosho ni moja katika sababu muhimu za kuwafanya wanyama wetu wawe na afya nzuri na waweze kutoa maziwa kwa wingi. Mhe. Mwenyekiti, suala hili kama litatendeka litaweza kupunguza homa kali sana kwa wanyama wetu na vile vile tutaweza kupunguza vifo kwa wanyama wetu, kwa sababu wanyama ikiwa hawashughulikiwi, hawatibiwi, hakuna utaratibu mzuri, matokeo yake wanyama hao wanaweza kufa mara moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mifugo ya asili ni kidogo na Serikali haiwapi nguvu wananchi kwa kukuza mifugo yao ndio sababu Zanzibar mara nyingi tunategemea kuchukua ng'ombe kutoka Bara au kununua ng'ombe kutoka Bara. Mhe. Mwenyekiti, suala hili hatulipendelei sana, tunapendelea

Wazanzibari kila jambo waweze kufanya wenyewe kwa sababu uwezo wa kufanya mambo haya wao wenyewe wanao, lakini kwa kuwa maana yake Wizara imewaweka nyuma na haishughulikii masuala haya kwa wafugaji wa asili ndio maana unakuta tunahitaji Zanzibar kuagizia ng'ombe kutoka Bara.

Mbali na hayo Mhe. Mwenyekiti, ni lazima kuwe na dawa za kuua wadudu hawa kupe na hizi dawa mara nyingi zinakuwa ghali sana, wananchi wanashindwa kununua na matokeo yake mifugo yetu inakufa kutokana na ukosefu wa dawa, dawa ni ghali na hazipatikani kwa urahisi, na kwa Unguja na Pemba mifugo yetu imeenea kila mahala. Kwa hivyo Mhe. Waziri, hilo ulielewe na nataka Mhe. Waziri nikuulize tu je kuna utafiti wowote uliofanyika ili kutaka kujua idadi ya ng'ombe tulionao hivi sasa hawa ng'ombe wa asili na vile vile wangapi wamekufa ng'ombe hawa kutokana na kukosa utibabu pamoja na homa kali zinazosababishwa na kupe ambao wanyama wetu wanakufa.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka nimuombe Mhe. Waziri, masuala haya ayazingatie na anipatie taarifa za kutosha kwamba sasa hivi tuna wanyama wangapi na wangapi wamefariki na kwa sababu gani?

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie suala la pili ambalo ni suala la mifugo tulilonalo hivi sasa, Wizara naamini imejitahidi vya kutosha kuwashawishi wananchi kufuga mifugo ya kisasa na baadhi ya wafugaji wanaendelea vizuri katika mifugo ya kisasa na wengine walikatisha njiani na ziko sababu bila ya shaka kwa nini wengine wakakatisha njiani, hii ni kutokana na kazi ngumu ya kuwalisha wanyama hawa, kwa sababu wanyama hawa sio wale wa asili ni wanyama au ng'ombe kutoka Bara ambao hawa matunzo yao ni makubwa sana kuliko matunzo ya wanyama wetu, kwa hiyo wana kazi kubwa ya kutoa huduma katika kuwalisha wanyama hawa, kwanza kwa kuweza kuwatafutia maji ya kutosha kwa ajili ya wanyama hawa, wanahitaji kuwa na mashamba ya majani, wanahitaji kuwa na chumvi ambapo lazima wapewe wanyama hawa na wanahitaji kuogeshwa kila siku. Sasa ukiangalia gharama zake Mhe. Mwenyekiti, ni kubwa sana, watu wetu wanashindwa kuweza kuzitekeleza huduma kama hizo, huduma hizi ni kubwa na nzito na ndio maana baadhi ya wafugaji wengine wamekatisha njiani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kama mambo yatakwenda vizuri ufugaji utakwenda vizuri na huduma zitapatikana za kutosha, wanyama hawa ni wazuri na wanaweza kutoa maziwa ya kutosha. Lakini kutokana na kushindwa na baadhi ya wafugaji kutoa huduma sahihi, matokeo yake mifugo inakuwa inakufa na wengine wanakata tamaa ya kuendelea. Wizara ya Mifugo baada ya kuona hali hii ni nzito na majukumu ni mazito wakafikiria njia nyengine ya kuweza kubadilisha kuwapa ng'ombe ambao huduma zake ni nzito na

matibabu yake ni mazito wakaona bora wafanye *cross breeding* kwa kuchukua ng'ombe wetu wa kienyeji na kuweza kupandishia na ng'ombe wale wa kigeni. Huu ni utafiti ambao waliofanya kutokana na wanyama wetu kupata homa kali na kufa kwa wingi na kushindwa kuweza kuwahudumia vizuri. Kwa kweli walichokifanya si kibaya ni kitendo kizuri kwa sababu hata ng'ombe wetu ukiwa utafanya kwa njia hizo za kupandisha kama kwa njia ya sindano au kwa njia ya ng'ombe wa Bara ambao ni wazuri ni suala muhimu sana.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile tuangalie tu kwamba pamoja na ufugaji huu kama ikiwa wanaendelea wale wale ng'ombe kutoka Bara tatizo ni habari ya hali ya hewa. Hali ya hewa yao ambayo walizoea wanyama kama hawa ni hali ya hewa yenye baridi na inapobadilika Zanzibar kuwa na hali nyengine ya joto hapo ndio inakuwa matatizo kwa wanyama hawa na hawawezi kustahamili kupe walioko katika nchi hii,kwa hiyo huduma zake zinakuwa nzito, lakini kwa kupata hii cross kwa kuchanganyisha mbegu mbili hizi ni sahihi kabisa. Lakini nilitaka nimwambie Mhe. Waziri, kwa nini huduma hii sasa inaanza kuvia hapa Zanzibar, Mhe. Waziri, ninahitaji kupata maelezo kwa nini suala hili halikuendelezwa Unguja na Pemba kuona namna gani wafugaji wanaweza kusaidiwa.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala jengine nilitaka niseme tu katika mifugo mengine ambayo tunaiendeleza mifugo ya asili ni mifugo ya mbuzi ni mifugo ya asili, kwa kule Pemba Wilaya ya Micheweni ni Wilaya moja wapo ambayo inashughulikia sana ufugaji wa mbuzi wa kienyeji, lakini ufugaji wa asili kwa mifugo ya mbuzi inazidi kupungua siku hadi siku kwa sababu mifugo ile ya asili ni moja wapo ambayo inawasaidia wananchi wa Micheweni kuweza kupambana na maisha magumu, inabidi mifugo yao waiuze ili waweze kupata mahitaji ya nyumbani. Kwa hiyo ninachotaka kusema katika suala hili ningelimuomba Mhe. Waziri, akawatembelea wafugaji wa Wilaya ya Micheweni na baadhi ya wengine walioko hapa Unguja ambao wanaofuga mifugo ya mbuzi wa asili.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile Mhe. Waziri, baada ya kufanya hivyo kutembelea na kuweza kupewa ushauri na kuweza kujua shida zao si vibaya ni jambo zuri, kwa hiyo ningelimuomba Mhe. Waziri, aweze kufanya hivyo, lakini vile vile ninamuomba Mhe. Waziri, pamoja na mifugo ya asili ya mbuzi vile vile wananchi wanahitaji kupata mbuzi ambao wa kisasa wanaoweza kutoa maziwa mengi. Je, Mhe. Waziri, ni lini utaratibu huu wa kuwahamasisha wananchi wa kuwa na mbuzi wa kisasa ambao wanatoa maziwa kwa wingi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo tuje katika suala zima la ufugaji wa kuku. Ufugaji wa kuku bado Zanzibar tunaagiza mayai kutoka nje, tunaagiza kuku

ambao Wazanzibari hawakubaliani nao na kuku ambao wanaletwa hapa Zanzibar. Hili ni suala muhimu sana na hii ni moja katika sababu ya kuwadharau Wazanzibari, hii ni moja. Kwa sababu Wazanzibari wako tayari kwa kufanya kazi za aina yoyote, lakini kutokana na hali hii kuleta makuku ya nje, mabovu, hayana *taste*, si mazuri kwa sababu ya kuwafurahisha wao, tujenge kwetu kwanza Zanzibar *first*, Zanzibar mwanzo halafu tutaangalia kwengine.

Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi Mhe. Waziri, hajawatendea haki wananchi wa Zanzibar. Wananchi wa Zanzibar ni mahodari kwa ufugaji na hizo ndio kazi zetu za asili, ufugaji wa kuku, ufugaji wa mbuzi, ufugaji wa ng'ombe ni moja katika shughuli zetu, lakini kutuletea mambo ambayo kutoka nje mnataka mututie maradhi sasa, hayo ni maradhi. Kwa hiyo ningelimuomba Mhe. Waziri, suala hili akalizingatia.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile nimpongeze Mhe. Waziri, kwa kazi ambayo aliyoifanya sasa katika utafiti ambao amekuwa kaufanya, namshukuru sana Mhe. Waziri, pamoja na watendaji wake kwa kuzingatia mbinu mpya ya uzalishaji wa mayai. Ninavyofahamu mimi katika maelezo yake Mhe. Waziri, tuna kuku wa namna nyingi hivi sasa ambao tayari tumekuwa nao. Utafiti huu hapa Zanzibar umechukua aina ya kuku wanaoitwa *australop, rhode island*,pamoja na *white legon* pamoja na kuku wa kienyeji kuku kishingo, utafiti huu ni mkubwa sana tena ni mzuri sana kwa sababu tunajifunza kutokana na makosa, makosa ya awali tulileta ng'ombe tukahisi ng'ombe kutoka Bara kutokana na *climate condition* ya Bara na hapa ni tofauti ng'ombe wale hawatufai, tukafanya *cross breeding* tukafanikiwa vizuri sana, na hivi sasa wamehisi kwamba kuchukua makuku kutoka nje na kuyaleta hapa ndani haya hayatusaidii.

Kwa hivyo wao wamechukua mchanganyo utafiti wao kwa kutumia kuku huyo *australop,island vane* na *white legon* pamoja na kuku kishingo wakachanganya mambo haya, matokeo ya utafiti wao ni mzuri sana uzalishaji wa kuku hawa utakuwa mzuri, kwa sababu unakuwa na mayai mengi, wanakuwa kwa haraka na ni wastahamilivu kutokana na maradhi mbali mbali.

Kwa hivyo mimi nampongeza Mhe. Waziri na ni walezi wazuri wa watoto wao, kuku hawa tunawaita machotara, machotara haya hutokana na kuku wetu wa asili mzao mmoja tu wanaweza kutaga mayai sitini na tano, mayai sitini na tano si kidogo kuku wetu wa kienyeji wa asili hawawezi kutoa kwa mpigo mmoja wa kutaga mayai 65, lakini yule kutokana na utafiti walioufanya sasa hivi kuku hawa chotara wana uwezo wa kutoa mayai 65 kwa mpigo bila ya kusita.

Mhe. Mwenyekiti, hao nimpongeze Mhe. Waziri, kwa nini alichokifanya na hivi sasa shughuli zinaendelea vizuri na majogoo yapo wanaotaka waende wakatafute majogoo hayo kwa ajili ya kuendeleza ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ninachotaka kumwambia, ili kuliendeleza hili suala ningelimuomba Mhe. Waziri, kukuza nia na madhumuni ya Wizara hizi mbili ya Kazi Uwezeshaji pamoja na Wizara ya Mifugo ni kuwanyanyua wananchi wetu kutokana na kipato chao kidogo, kuwanyanyua ili wawe na kipato kikubwa na waweze kushiriki katika mambo mbali mbali ya uzalishaji. Kushauri basi ningelimwambia Mhe. Waziri, tunahitaji kuwa na *incubators* ambazo tutakuwa na mayai kwa wingi, tunaweza kutia katika *incubators* zetu kwa ajili ya uzalishaji.

Kwa hivyo ningelimuomba Mhe. Waziri, suala hili alitekeleze kwa kuwapitia wananchi, kuwashauri na kuwahamasisha waweze kununua *incubators* au kama zitakuweko mahala *incubators* kwa ajili ya kuwekea mayai ya kuzaliwa vifaranga hili ni jambo la msingi. Kwa hivyo hili ni suala muhimu na vijana wetu watashawishika wataanza kupunguza matumizi ya dawa za kulevya watajishirikisha katika kazi za uzalishaji, Zanzibar sisi tuko mahodari kwa kazi kama hizi za uvunaji wa kuku.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Na kwa upande wangu mimi kuna mambo mawili tu yamenigusa katika Wizara yangu, moja ni la soko la mwani na pili ni suala la kuku kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, nikianzia na suala la masoko ya kuku kutoka nje hapa kwetu Zanzibar, kilio cha wafugaji wa kuku Zanzibar hatukuanza kukisikia leo au jana, katika mazungumzo hapa katika Baraza la Wawakilishi kwa uchungu kabisa, lakini sisi tumepata habari hizi mapema katika mwaka 2011 na Serikali ilichukua hatua madhubuti kwa kuunda kamati maalumu ambayo ilishirikisha Mawaziri kutoka Wizara tatu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Afya na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, tukishirikiana na watendaji wetu tulifanya kazi ya kina kabisa kuangalia namna gani biashara ya kuku imekuwa *affected* na masuala mazima ya ufugaji kuku wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Salmin Awadh, kwa kuweza kutoa *data* nzuri kabisa, kafanya utafiti na katoa *data* nzuri kuonesha namna gani mchango wa wachangiaji walivyochangia kuhusu masuala ya uagizaji wa kuku kutoka nje. Katika *data* ambayo ameitoa

Mhe. Salmin ni sahihi kabisa kwamba tunahitajia angalau tupate tani 585 kwa muda wa mwezi mmoja, kwa mwaka tunahitajia tani 7020 na wafugaji wa Zanzibar wana uwezo wa kuuza tani 163 tu kwa mwezi ambao katika hizo tani karibu 90 ni kuku wa aina ya kizungu au *broilers* na waliobakia ni kuku wa kienyeji. Kwa hiyo utakuta kuna nakisi ya tani 369 wa nyama ya kuku inahitajika Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikumbushe kwamba utafiti huu au *data* hii inatokana na kwamba kila familia moja ile kilo tatu tu za nyama ya kuku kwa mwezi, yaani kila wiki mbili familia moja ya Mzanzibari wale kilo moja na nusu ya kuku kwa mwezi kilo tatu ndio tunahitajia tani 585, lakini ikifika Wazanzibari wakahitajia kula angalau kilo tano tu kwa mwezi kwa kila familia utakuta itahitajika zaidi ya tani 800 kwa mwezi, kwa bahati mbaya tunazalisha kuku idadi ndogo sana, sasa kuku kutoka nje ni tani 54 tu kwa mwezi, kwa hivyo sisi tunaagizia tani 648 ya kuku kutoka nchi za nje. Sasa basi baada ya kufanya utafiti huu ni njia gani tutaweza kumsaidia Mzanzibari mfugaji.

Mhe. Mwenyekiti, tumeangalia kwa kina, kwanza kulikuwa na malalamiko ya kwamba kuku wanaoingia hapa kutoka nje wako chini ya viwango. Kwa hivyo hapa pana chombo madhubuti ambacho kinaangalia viwango vya vyakula, madawa na vipodozi vinavyoingia nchini, kwa mujibu wa sheria, Wizara ya Afya imeunda bodi ya viwango ni bodi ya madawa, vyakula na vipodozi kuangalia namna gani wao walikuwa wanafanya utafiti wao au uchunguzi wao. Tulichukua *sample* ya kuku walioingia nchini na tukawafanyia utafiti zaidi na zaidi, tukagundua kwamba kuku wanaoingia nchini wote wako katika viwango vinavyohitajika vya kimataifa, hapakuwa na sababu yoyote ya kuweza kuzuia kuku hawa kutokana na viwango vyake, viwango vyake ni vya hali ya juu kabisa hasa ukilinganisha na hali halisi ya kuku ambao sisi wenyewe hapa Zanzibar tunawazalisha. Laiti mtalii yeyote ambaye kwamba atatembelea soko la Zanzibar na kuangalia machinjio ya kuku wa Zanzibar wanavyochinjwa huyo mtalii atapagawa hapo hapo, kwa kweli mazingira ya kuchinja kuku katika Marikiti ya Zanzibar yanatisha, na kwa bahati nzuri au kwa bahati mbaya kuku ambao sisi wenyewe hawapimwi au hawapitii katika hii bodi ya vipodozi, laiti kuku hawa wakienda kupimwa katika hii bodi naamini kwamba kutakuwa na mushkeli mkubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambayo ndio inahusika katika masuala ya biashara, Serikali ya Tanzania imeweka saini katika mkataba wa *World Trade Organization*, unapozuia biashara yoyote kutoka nchi nyengine kuingia Zanzibar bila ya kuwa na misingi madhubuti unakwenda kinyume na ule mkataba ambao Serikali ya Tanzania imeridhia, mkataba wa kibiashara wa dunia katika *WTO* ambayo inampa nafasi kila mtu

duniani aweze kula au kutumia chochote anachokitaka katika nchi yoyote ulimwenguni, unapozuia kuku hawa wasiingie Zanzibar bila ya sababu za msingi ni kwenda kinyume na mkataba huo ambao Serikali ya Tanzania imeweka katika *WTO*.

Tunaweza kuzuia kuku hawa wasiingie nchini kwa kuweka ushuru mkubwa. Lakini suala la kuongeza ushuru mkubwa ni la muda mfupi tu si la muda mrefu, nadhani kuna *tariff barriers***.** Kwa hivyo, sisi tulilolifanya ni kuweka viwango vya juu vya ushuru wa kuku wanaoingia Zanzibar ili kumlinda mfugaji wa Zanzibar, ninaloliomba chini ya usimamizi wa Wizara ya Fedha, *TRA* wahakikishe kwamba kuku wote wanaotoka nje wanaoingia Zanzibar wanalipa ushuru ambao serikali imeweka, ushuru mkubwa umewekwa ili kuweza kumhifadhi huyu mfugaji wa Zanzibar.

Kwa hivyo, hatuna sababu ya msingi ya kuweza kuzuia kuku hawa wasiingie Zanzibar, watalii wote au wengi wanaokuja hapa wanahitaji kuku hawa wa kutoka nje kuliko kuku wanaozalishwa Zanzibar. Lakini suala kubwa au changamoto kubwa tuliyonayo sisi ni kwamba, kuku wetu ambao tunazalisha Zanzibar ni ghali sana, sio ghali, ni ghali sana hata inampelekea Mzanzibari mwenyewe kutomiliki kutumia kitoweo cha kuku. La kushangaza zaidi tufanye sisi wenyewe upelelezi tuangalie kuku yule yule anauzwa shilingi elfu sita lakini akikaangwa tu anauzwa shilingi 14 elfu yaani kila ubavu wa kuku unauzwa shilingi elfu saba. Hii ni asilimia zaidi ya mia, kuku huyo huyo akifanywa mshikaki kuku mmoja huyo aliyenunuliwa shilingi elfu sita anauzwa shilingi 12 elfu. Je, hii ndio biashara halali, ndivyo biashara inavyotakiwa?

Mhe. Mwenyekiti, suala zima hapa ni kuona kwamba vipi tutaweza kumpatia mlaji, tusimtetee tu mfugaji kuku, tumtetee vile vile na mlaji kuku. Mzanzibari anataka kula kuku aliyekaangwa na chipsi, ananunua kuku mmoja shilingi 14 elfu bila ya mwenyewe kujua wakati huyu muuzaji chipsi kanunua shilingi elfu sita anamuuza shilingi 14 elfu, mshikaki ule kanunua shilingi sita anamuuza shilingi 12 mbona hamuwatetei Wazanzibari hawa wanaokula kuku. Lazima tuangalie biashara huwezi kununua kitu shilingi elfu sita ukauza shilingi 14 halafu unamtetea huyu tu, hakuna hiyo tufanye *balance,* mlaji kuku na mfugaji tuangalie wote kwa usawa kabisa tuone kwamba namna gani tutaweza kuwasaidia na kuwalinda. Kwa hivyo, suala zima la makuku linatakiwa lifanyiwe kazi zaidi, sasa tunaomba mtupe nafasi zaidi serikali.

Suala hili tumeshalianza na tunaliendeleza kwa namna gani tunamsaidia mlaji kuku na namna gani tutamsaidia mfugaji ili kila Mzanzibari aweze kumiliki kula kuku. Dunia nzima kitoweo cha kuku ndio kitoweo rahisi chao, lakini Zanzibar ndio kitoweo ghali chao, mambo ya ajabu. Haya ni mambo ya ajabu

sana lazima kila Mzanzibari aone kwamba kitoweo cha kuku ni rahisi kuliko chengine chochote kwa sababu ndivyo ilivyo. Nasema kwamba nafasi ya kufuga ipo, soko lipo, nakisi ipo kwamba tunahitajia tani karibu 400 za kuku kuzalishwa Zanzibar. Kwa hivyo, jitihada itafanyika kuona kwamba wafugaji wa kuku Zanzibar wanafuga kuku na nyama ya kuku itapatikana kwa bei rahisi, lakini suala la kuzuia kuku kutoka nje wasiingie Zanzibar ni suala la muhali kabisa, tutakwenda kinyume na mikataba ambayo sisi wenyewe tumeiweka kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumaliza hiyo kadhia ya kuku sasa hivi naomba niende katika suala zima la mwani. Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema awali hapa siku za nyuma kwamba Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi inashughulika sana katika masuala ya upandaji wa mwani na uzalishaji, lakini masuala ya masoko ya mwani ni suala ambalo moja kwa moja linashughulikiwa na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Katika suala hili tunashirikiana kwa dhati kabisa baina ya Wizara mbili hizi kuona kwamba Wazanzibari wapate bei nzuri ya mwani kuliko ilivyo sasa.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii inastahili pongezi kubwa sana kwamba imeweza kusimamia suala zima la upandaji mwani, ukiangalia takwimu kuanzia mwaka 2007 zilikuwa zikizalishwa tani 8,485 kwa mwaka huo, ikapanda 11,000 mwaka 2008; mwaka 2010 ikenda 11,900; mwaka 2011 ikenda tani 13,000 tukafika mwaka 2012 tani 15,000 na ushei. Hii inaonesha wazi kwamba Zanzibar kwa Afrika nzima ndio nchi pekee inayotoa idadi kubwa ya mwani, nchi jirani kama vile Mozambique ambako ni Msumbiji huko, Madagascar, Mauritius, Kenya zinatoa idadi ndogo sana ya mwani. Mwani unaotoka Tanzania Bara ni takriban tani 1,000 hizi nazo zote hukimbilia katika masoko ya Zanzibar.

Kwa hivyo katika tani 15 elfu tulizofika Zanzibar tani 1,000 inatoka Tanzania Bara. Sasa basi, ukiangalia kwa ufupi ni kwamba bei ya mwani imeshuka na sisi tulichunguza tulifikiri kwamba wale wanunuzi wa mwani nchini wanawalazia wananchi au wanawadhulumu, tukafanya uchunguzi wa kina tukaona kwa kweli biashara ya mwani inakwenda vizuri isipokuwa suala kubwa ni kwamba uzalishaji wa mwani duniani umekuwa mkubwa kuliko matumizi ya mwani. Baya zaidi kwamba Indonesia wanatoa mwani aina ya *Cottonii* mwingi zaidi sisi tunatoa *Spinosum*, *Spinosum* sisi tunatoa nyingi sana ambapo bei yake ni ya chini *cottonii* yenye bei kubwa zaidi Zanzibar haioti vizuri.

Sasa Indonesia katika muelekeo wao wamepanga ifikapo mwaka 2014 watatoa tani milioni kumi za mwani nchini mwao mwani mbichi. Hiyo ina

maana kwamba, huko tunakokwenda hatari zaidi kwa sababu mwani utakuwa ni mwingi matumizi ni yale yale. Nini juhudi za serikali katika suala hili?

Naomba niwaarifu Wawakilishi wote pamoja na wananchi kwa jumla kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajua wazi kwamba mwani ni bidhaa muhimu sana kwetu sisi, kwa sababu Zanzibar tuna bidhaa za kilimo nne tu tunazopeleka nje. Kwanza ni karafuu, pili mafuta ya karafuu, mwani na raba. Sasa basi, mwani ni suala muhimu sana kwa serikali yetu, tunasimamia tuone kwamba masoko haya hayaathiriki kwa kiwango kikubwa. Kwa hivyo, juhudi imefanyika kubwa tu na hivi sasa sisi tulikuwa tukiomba *UNIDO*, hili ni kama Shirika la kimataifa tumeiomba *UNIDO* itusaidie namna gani tutaweza kuweka viwanda vya kusarifu mwani nchini. Kwa bahati nzuri tumezungumza na *UNIDO* miezi mitatu tu iliyopita, *UNIDO* imechukua ombi letu kwa umuhimu mkubwa sana.

Hivi ninavyokwambieni jopo la mabingwa kutoka *UNIDO* wapo Zanzibar wamekutana na mimi siku ya Jumatatu ofisini kwangu, wamekwenda na Pemba wamekaa leo ni siku ya tano na *Inshaallah* saa nane mchana nitakutana nao ofisini kwangu wakitokea Pemba. Jopo hili la mabingwa kutoka *UNIDO* mmoja wao ni Mwenyekiti wa wazalishaji mwani duniani ambaye ni mtu mzuri sana, mimi nilikutana naye Indonesia katika mkutano wa mwani mimi mwenyewe nilipomuona nilishangaa sana. Kwa sababu ni mtu muhimu na ni mtu mkubwa sana akafika Zanzibar na amekuwa Pemba kwa muda wa siku tano, na Zanzibar siku mbili kuangalia namna gani mwani unavyozalishwa, namna gani kinamama wanaofanya kazi hii ambao ni wengi karibu asilimia 90 wanavyoathirika na suala zima la mwani na bei ya mwani inavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, tunaomba *UNIDO* watusaidie kuwekeza viwanda vya kuweza ku-*process* mwani Zanzibar, na wao wametwambia kwamba watafanya kazi hii kwa umuhimu mkubwa, *very serious* kuona kwamba tunawasaidia Wazanzibari ili mwani wao uwe *process* hapa hapa Zanzibar bila ya kwenda nje na kuuza *raw material*. Naomba Wazanzibari wote tuwe wastahamilivu wakati *UNIDO* wakifanya kazi hii. Leo saa nane nitapokutana nao tutajua muelekeo mzima wa suala hili. Lakini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nataka niwahakikishie Wazanzibari wote kupitia kwa Wawakilishi wetu hapa kwamba serikali inalifanyia kazi suala hili kwa umuhimu mkubwa kuona kwamba Wazanzibari, wengi wao wakiwa kinamama wanapata faida kubwa kutokana na zao la mwani. Tusingependa kuona zao la mwani linapungua, tungependa kuona idadi ya tani za mwani nchini zinazalishwa zaidi na zaidi, na wizara yangu itafanya kila bidii inayowezekana kuona kwamba viwanda vya mwani vinaanzishwa Zanzibar ili tuweze ku-*process* mwani hapa hapa na tuweze kuzalisha ajira Zanzibar.

Kwa hivyo, naomba mtupe kila baraka zenu mtuombee dua *Inshaallah* katika huu mwezi mtukufu wa Ramadhani Mwenyezi Mungu atutakabalie juhudi hizi za serikali zifanikiwe ili wananchi wetu wapate kufaidika na zao zima la mwani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na nawatakia kila la kheri nawaombea sana ndugu zangu Wawakilishi tuwasaidie Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi ili bajeti yao hii ipite, kwa sababu wana kazi kubwa mbele yetu inayokuja. Tuna shughuli ya mwani, tuna shughuli ya kuku na tuna shughuli ya dagaa. Kwa hivyo, tutayafanyia kazi tunaomba mtupe moyo.

Sasa hivi dagaa kuna wazalishaji zaidi ya 25 elfu na hii ni moja katika shughuli ambayo tunaifanya vile vile kuitafutia soko zuri kabisa. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana. Wahadhassalaamu Alaykum.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu Azza Wajalla kwa kutufikisha hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema kabisa.

Pili, niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kutoa hoja mbali mbali na hoja zile zilikuwa maana yake ni kujenga sio kubomoa. Vile vile nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wangu kwa kazi kubwa anayoifanya na tukiwa pamoja katika kutekeleza majukumu yetu ya kila siku pamoja na Katibu Mkuu na watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, nami nijaribu kujibu baadhi ya hoja ambazo zimeletwa na Waheshimiwa Wawakilishi ili basi kufahamu dhana kubwa ya wizara yetu na mambo ambayo tunaendelea kuyafanya kwa hivi sasa. Kwanza kabisa kabla ya kusahau na mimi niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mpendae naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti, la pili niwaombe Waheshimiwa wote watuunge mkono na waunge mkono hoja hii ili tutekeleze majukumu yetu, watupitishie bajeti yetu ili tutekeleze kazi kubwa tuliyokuwanayo. Nafikiri punde tu tumemsikia Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko jinsi gani alivyopanga mipango thabiti ya kuweza kuwainua wakulima wa mwani na wengineo, manaake wapo wa Kusini Pemba wananisikiliza kwa karibu zaidi wakulima wa mwani.

Mhe. Mwenyekiti, labda mimi nianze tu kujibu baadhi ya hoja za baba mkwe wangu Mhe. Mbarouk Wadi Mussa alizozitoa jana Mtumbatu wa juu. Mhe. Mbarouk alitaka kujua baadhi ya vifungu, kifungu nambari 2202701 na

220711, vifungu vya matengenezo madogo na makubwa. Nataka kumwambia ni kweli tumehamia katika jengo jipya, imara na zuri kabisa, lakini matengenezo makubwa yale yalikuwa kujenga uzio ambao waliuita ule uzio wa mabati kama bado hatujahamia. Nataka kumwambia tayari tumehamia kwa nguvu zote na tunatekeleza majukumu yetu katika nyumba ile, lakini matengenezo makubwa yale wafadhili hawakutupa pesa kujenga ukuta, tulitaka tujenge ukuta pale kwa sababu yale mabati tuliyaweka hatujayatoa kuepusha mambo mengi, kwanza kuepusha wizi lakini la pili kuepusha wale jamaa zake wasilete punda wengi mle ndani. Kwa sababu hata jana tumekuja tuliporudi kutoka hapa kwenda kujadili hizi hoja za Waheshimiwa Wajumbe basi tumekuta punda wawili wameingia pale ndani. Sasa ile ndio madhumuni yake tunajenga ukuta kuhifadhi mambo mengi pamoja na hayo. Kwa sababu pia punda ni moja kati ya mifugo yetu sisi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha matengenezo madogo madogo. Kifungu hiki nafikiri hata nyumbani kwako kunaweza kutoka *bulb* zikaungua, sinki zinaziba, hii ndio maana yake matengenezo madogo madogo ambayo yanaweza yakafanyiwa kazi, lakini tusi-*query* matengenezo madogo madogo wakati vitu havikai kwa kudumu. Ni kweli nyumba mpya lakini je, *bulb* haziungui, karo hazizibi na vitu kama hivyo, *AC* zinaweza zikabomoka mara moja, ile ndio maana yake matengenezo madogo madogo.

Sasa hivi niende moja kwa moja kwa shemegi yangu Mhe. Ismail Jussa Ladhu aliyetaka kujua kesi ambayo inaendelea pale na meli zile za Bahari Kuu. Kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mkurugenzi wangu Zahor El-kharoos kwa kazi kubwa sana ambayo anaifanya na ufuatiliaji makini ambapo yupo pamoja na sisi kila wakati na ninamwambia tu asivunjike moyo, pamoja na kuwa madongo mengi yanakuja katika kufuatilia kesi hii maana mpaka vitisho anapata, lakini namwambia asivunjike moyo. Sisi tuko pamoja naye na suala hili nimeshalitolea taarifa polisi kwa *DCI* jinsi wanavyolifuatilia.

Mhe. Mwenyekiti, suala la uvuvi haramu katika Meli ya Haw Kun**.** Hili alisema sana Mhe. Jussa jana na mimi nataka kumjibu kama ifuatavyo: Meli ya Haw Kun yenye nambari 168 na imesajiliwa katika Bahari Kuu na ndiyo iliyopelekea malalamiko ya meli hii katika Tume ya *IOTC (Indian Ocean Tuna Commission)*. Kama ulikuta kwenye mtandao basi hii kesi tulipeleka sisi pale na tume hiyo imechukua malalamiko yetu ambayo Mhe. Jussa aliipata kupitia mtandao. Meli hii imesajiliwa Taiwan imefahamika kuwa zilizuiliwa katika maji ya Tanzania. Meli hizi ziligundulikana zinavua katika bahari yetu ya Tanzania, na Mkurugenzi wangu basi alichukua hatua ya kuuliza, kwa sababu kuna chombo maalum ambacho kina-*monitor IAS*. Hiki ni chombo ambacho kina *monitor* safari nyingi za meli ambazo zinakuwa bahari mbali mbali.

Niende *IAS* meli hizo zinapatikana katika mamlaka ya kupitia kwenye *program* ya kukabilana na uvuvi haramu ukanda wa Kusini wa Afrika, ambazo nchi hizo ni Kenya, Mozambique, Comoro, Tanzania na Seychelles ni wanachama wa programu hiyo. Mwendo wa *IAS* wa meli ya Haw Kun nambari 68 ulionesha kuwa meli hiyo inafanya kazi ndani ya ukanda wa uchumi wa Tanzania kuanzia mwishoni mwa mwezi Oktoba hadi mwishoni mwa mwezi wa Disemba 2012. Meli hiyo haikuwa na leseni iliyoruhusika kuvua kwenye maji ya Tanzania. Katika kipindi hicho mwenendo wa *IAS* ulionesha meli hiyo ilifanya uvuvi ndani ya ukanda wa uchumi wa Tanzania kuanzia tarehe 12 – 18 Juni, 2011; tena tarehe 23 ya mwezi huo halikadhalika meli hiyo haikupatiwa leseni ya kihalali kupitia katika mamlaka yetu ya Bahari Kuu. Lakini meli hizo zilikuwa mbili, moja ilisajiliwa Taiwan na moja imesajiliwa Seychelles ambayo ilikuwa ikipepea bendera ya Seychelles.

Mamlaka yetu ilipeleka barua za uvuvi wa nchi mbili hizo na kuomba maelezo thabiti kuwa meli hizo ni za nchi gani na nchi husika na kama mfumo wa *VMS* na meli hizo imeonesha kuwa zimeingia katika ukanda wa kiuchumi wa Tanzania tarehe iliyotajwa hapo juu. Kutoka katika mamlaka ya Taiwan yalikuwa ni kwamba, meli ya Haw Kun nambari 68 ni yao na iliingia katika maji ya Tanzania katika moja iliyotajwa hapo juu. Mkurugenzi wangu alichukua hatua thabiti kuwasiliana na Mamlaka ya Seychelles na Taiwan na vile vile wakajibu kwa barua ambayo tayari wametuletea, lakini kutokana na kuona wametuletea kibali nambari 859 ambapo wamesema ni tayari tumewapa sisi baada ya kuangalia orodha ya vibali tulivyovitoa havimo katika orodha yetu vyote viwili, tulichukua hatua tukaviangalia nani aliyetoa na kulikuwa kuna jina la mfanyakazi wetu mmoja ambaye anaitwa Damian Boniface Chando, ndiye aliyetoa vibali vile kwa kushirikiana na mfanyabiashara mmoja ambaye anaitwa El-Sheybaan. Hawa ndio waliotoa vibali hivyo na tulivigundua baadae katika kufuatilia baada ya vile viwili lakini tulikuta vibali kumi tayari zimeshatolewa.

Lakini Mkurugenzi wetu aliripoti ofisini tukachukua hatua ya kumsimamisha kazi kwanza, lakini baada ya kumsimamisha kazi tulifungua kesi katika Kituo cha Polisi Fumba ili kuweka hatua za kisheria kuweza kuchukuliwa. Vile vile tulienda tena katika *IOTC* kufungua kesi kule lakini kabla walitutaka kwanza kesi yetu iende, kabla ya kesi yetu kwenda Mkurugenzi aliwaandikia polisi siku ya tarehe 13 mwezi wa sita (6) akitaka kujua mwenendo wa kesi umekuwaje. Lakini polisi walijibu tarehe 19 Juni, kuwa bado uchunguzi wa kesi unaendelea na hawajampata El-Sheybaan na kwa sababu yuko India kimatibabu.

Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri mimi nasema Mungu hamfichi mnafiki, El-Sheybaan alikuja kwa Makamu wa Pili wa Rais kuomba *transaction* ili tumpe

kibali kuweza ku-*shift* wale samaki. Tukamwambia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais huyu ndiye tunayemtafuta, kumbe mna kesi naye? Ndio tuna kesi naye, basi tukachukuana tukaenda polisi pale tukamaliza akachukuliwa *specimen*, na juzi nimefuatilia mimi mwenyewe kwa *DCI* tumeona mambo yamekwenda vizuri na kesi ile imepelekwa Dar es Salaam katika utambulisho wa saini na kila kitu. Hicho ndio kitu ambacho kimeweza kufanyika, na kesi hiyo nataka kusema sasa iko polisi kwa hatua zaidi imeondoka katika mikono yetu sisi na tumechukua hatua kubwa zaidi.

Mhe. Mwenyekiti suala la pili labda Mhe. Jussa alitaka kujua yale makusanyo ambayo yako pale, makisio ya makusanyo ya Bahari Kuu. Makisio ya makusanyo ya Bahari Kuu ni shilingi 2,077,000,000 lakini mapato halisi ni kidogo kama ulivyoyaona katika kiambatanisho nambari 11, ni shilingi 100,046,000. Haya mapato ambayo tayari yameshagawanywa, mapato haya jibu lake ni makisio ambayo tayari yameshagawanywa na makisio haya yanagawanywa mara tatu, mara tatu yenyewe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapata asilimia 20, ambayo ndio hiyo iliyokuwemo kwenye kiambatanisho chetu. Lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapata asilimia 30 na Mamlaka yenyewe inapata asilimia 50 ili iweze kujiendesha. Sasa mchanganuo unakuwa kama ifuatavyo:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika asilimia 20 imepata shilingi 432,802,044; SMT ambayo imepata shilingi 649,203,660 na Mamlaka yenyewe imepata shilingi 1,082,006,100. Huo ndio mchanganuo halisi ambao umeweza kupatikana. Sasa unaweza kuuona kuwa ni kidogo zaidi pale katika kitabu, kwa sababu ule ndio mgao wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulivyokuwa baada ya kutoa migao yote kwa pamoja, lakini pesa zenyewe ndio zilikuwa zile shilingi 2,077,000,000.

Naomba tena kujibu hoja ya Mhe. Asaa Othman Hamad ambaye ni Mwakilishi wangu katika Jimbo la Wete. Yeye alitaka kujua leseni ngapi za halali zimetolewa kwa kiasi gani, leseni ngapi za kughushi zimepatikana na kupoteza kiasi gani mhusika huyu atajwe, lakini mhusika nasema nimeshamtaja tayari.

Mwaka 2012/2013 Mamlaka imeuza leseni 38 zenye thamani ya shilingi 2,164,530,600. Leseni za kughushi zilipatikana kumi zenye thamani ya shilingi 167,680,000; mtuhumiwa au watoaji leseni hizo ni Afisa Mdhibiti wa Mamlaka Bwana Damian Boniface Chando na leseni hizo zilionesha kuwa zimenunuliwa na Bwana Ahmed El-Sheybaan, hapa tuna mtu mmoja Ahmed El-Sheybaan huyu ndiye ambaye anaelekea alikuwa aki-*monitor* hili suala na kuweza kuzinunua hizi kwa njia ya kughushi. Mimi nichukue fursa hii

kuwaomba wenzangu wa polisi wamshughulikie sana vyenginevyo atatutia *short* za haraka sana.

Lakini vile vile nimjibu kaka yangu kipenzi cha Konde Mhe. Suleiman Hemed Khamis, yeye alitaka kujua tu mpango wa uvuvi wa Bahari Kuu ili kukuza uchumi wa Zanzibar na kukuza kipato cha moja kwa moja. Jibu ni kwamba, mpango wa kuanzisha mradi wa kuendeleza uvuvi wa Bahari Kuu kwa kuwapatia mafunzo ya uvuvi wa Bahari Kuu wavuvi wa Zanzibar ambao bado hawana ujuzi wa kuvua.

Katika suala la msingi nililokuwa nikijibu nyuma kidogo nilijibu kuhusu ile meli ya majaribio ambayo tunataka tuweze kuwapatia vijana 30 kuweza kuwafundisha. Nimesema vijana wale tutaanzia kwa *Form IV* kwa sababu zina *electronic* ndani yake na mambo mengi sana, zina nyavu za *troll*, nikizungumza nyavu za *troll* ni zile za kukokota sizungumzii zile nyavu ambazo zina uvuvi haramu. Nataka kuzungumzia vitu vya mashine ambavyo vimo mle ndani, tumesema tuanzie kwa vijana waliomaliza *Form IV* kwa sababu tunasema tunaweza tukawafundisha wakaweza kufundishika.

Lakini hatumkatazi mtu mwenye kiwango cha elimu ile ya kuanzia *Form IV* kuja juu akaweza kujiunga. Sasa hii tumesema tunaanzia baadae serikali inaweza ika-*inject* pesa, wengi walilalamika jana Idara ya Uvuvi imetiliwa shilingi milioni mia moja ni kidogo hatuwezi kwenda, ni kweli hata sisi wenyewe maana yake ukiniambia mimi naweza nikapata hata *pressure* hatuwezi kwenda, lakini tuache tujaribu baadae tuone serikali katika mfuko mkubwa ita-*inject* kiasi gani cha kuweza kufanya mambo yale.

Taasisi zinataka kupewa mikopo nafuu, tuna taasisi ambazo tayari tumezilenga kutoa mikopo nafuu kwa wavuvi wetu. Mimi nasema tunataka tuondokane na ule uvuvi wa kuvua pondo au ngalawa za pondo tuondokane nao, ingawaje serikali imetuwezesha kuanzia mwaka 2005 kutoa mashine mbali mbali, sasa tuanze kwenda mbali zaidi na tukifanikiwa itakuwa hilo ni jambo jema na tutatumia samaki wetu au rasilimali hii kwa haraka zaidi.

Labda pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Waziri wa Biashara ya kuku wa Peduu, ukweli kuku wa Peduu hatuwezi kuwazuia hivi sasa, lakini tuwe na mbinu mbadala za kuweza kufanya. Hata mimi nasema kama mimi Mwakilishi basi wananchi wangu tayari wameshanilalamikia muda mwingi kuwa kuku wale hawawataki, lakini kuna biashara huria ambayo inafanywa. Labda tutakaa na wenzetu Wizara ya Biashara kujua ni jinsi gani ya kuweza kufanya au kudhibiti kama wenzetu Bara wamefanikiwa na kudhibiti hali hii. Hali hii imedhibitiwa vipi, wamefanya mpango wa kuzalisha kwa wingi kuku wa ndani na hatimaye basi hawaletwi wa nje.

Mimi nafikiri tukae pamoja tuweze kujua, hii nyumba tunayojenga tunajenga nyumba moja sote, kwa nini tuweze kuvutiana fito? Hatuwezi kuvutiana fito wakati tunajenga nyumba moja, tukaeni pamoja kila Mwakilishi ana dhima ya kuweza kuishauri Serikali juu ya jambo hili au jambo lolote ambalo analiona litapelekea Serikali yetu kuendesha vizuri, pamoja na wizara yetu kuendesha vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, nijibu hoja za Waheshimiwa Wawakilishi walio na vikundi vyao mbali mbali waliotaka kutembelea na waliotaka kusaidiwa. Mimi nawaambia tu baada ya bajeti hii tena mniunge mkono kwenye bajeti hii muipitishe haraka ili mimi niweze kuja kule mniwezeshe nije. Mnajua mimi Mnyamwezi napenda kazi. Sasa niweze kuja kule kuwatembelea na tuone njia gani tunaweza tukashauriana na tukaweza kuwasaidia vikundi mbali mbali.

Nafikiri ikimalizika bajeti hii naomba *list* ya Waheshimiwa wote waje hata mkitaka tukimaliza tu Baraza basi mimi niko tayari kuja kule na Mhe. Waziri wangu tukafanya ziara tukawaona na tukaweza kuwasaidia. Hilo halina mashaka, zaidi tunachokuombeni mtuunge mkono mtupitishie bajeti hii na Mhe. Mwenyekiti, nataka wote niwaamkie Waheshimiwa Wawakilishi shikamooni! Mtupitishie bajeti yetu wala msiwe na wasiwasi kazi tutaifanya ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwashurukuru sana na kukushukuru wewe kwa kunipa muda huu mdogo. Lakini Mhe. Waziri wangu atakuja kuendelea na kuwajibu. Lakini nawaomba sana Waheshimiwa tuunge mkono. Mimi naunga mkono hoja asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwanza na mimi sina budi kumshukuru Allah kutufikisha asubuhi hii kuwa wenye afya na uzima na wenye furaha.

Mhe. Mwenyekiti, nimesimama hapa ili kufanya majumuisho kwa masuala mbali mbali ambayo wametoa Waheshimiwa Wajumbe ambayo yalikuwa na nia nzuri ya kujenga, kushauri, kutoa maoni na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kutoa shukurani kwa *Allah* kwa kutukutanisha mara nyengine tena kuwa wazima wenye afya nzuri.

Pili napenda kutoa kuchukua fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi pamoja na Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yenu. Michango yote iliyotolewa ilikuwa na nia ya kunisaidia kama nilivyosema awali, mimi pamoja na watendaji wa wizara yangu katika kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi wa kufikia malengo ambayo tuliyokuwa tumejipangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba uniruhusu nitoe shukurani zangu vile vile za dhati kwa kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kutoka Baraza la Wawakilishi iliyomaliza muda wake chini ya Mwenyekiti wake mama Asha Bakari Makame. Kwa ushauri, nasaha na maelezo kwa aliyoyatoa katika kuelekeza wizara yangu ili kufikia malengo yetu kwa kuwahudumia wafugaji wavuvi na wakulima wa mwani.

Wizara yangu itafuata maelekezo ya kamati kwa kadri ya uwezo wetu. Mhe. Mwenyekiti, pia naomba kutoa shukurani zetu kwa Mhe. Makamo Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari Mhe. Abdalla Moh'd Ali ambaye hii leo au jana alisimama kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mlinde Mabrouk Juma.

Aidha natoa shukurani zangu za dhati kwa Wajumbe wote wa Kamati kwa kutupatia ushauri na maelekezo ambayo yamechangia sana katika kupatikana kwa ufanisi katika yale mambo yaliyofanywa vizuri.
Mhe. Mwenyekiti, michango iliyotolewa na kamati hii ilijikita katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza kushirikiana na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika ili kuweza kuwapatia mahitaji wajasiri amali. Lakini vile vile ilijikita katika kwenye wavuvi wa Zanzibar kukatishwa tena leseni wanapokwenda Tanzania Bara. Vile vile kuongeza bajeti ya Doria, kuanzishwa Chuo cha Uvuvi, bajeti ndogo ya wizara, kuwawezesha wavuvi kwenda kuvua kwenye bahari kuu. Kamati imeridhishwa na utendaji wa wizara kwa ujumla na hasa Idara ya Utabibu wa Mifugo, Idara ya Mazao ya Baharini na Idara ya Uzalishaji Mifugo. La mwisho ilikuwa la ubunifu wa ukusanyaji wa mapato hasa kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba ya wizara yangu ilichangiwa na jumla ya Wajumbe 27. Lakini nafikiri itakuwa ni 28 kwa sababu wengine wameleta hivi asubuhi. Pamoja na Mhe. Naibu Waziri kati ya hao imekuwa ni Wajumbe 20 waliochangia moja kwa moja na Wajumbe saba au nane walichangia kwa maandishi. Naomba uniruhusu niwataje wale waliochangia hotuba hii nikianzia na waliochangia moja kwa moja kama ifuatavyo:-

Mhe. Ali Salim Haji
Mhe. Asha Bakari Makame
Mhe. Subeit Khamis Faki
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Ismail Jussa Ladhu
Mhe. Mwanajuma Faki Mdhachi

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
Mhe. Saleh Nassor Juma
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa
Mhe. Rufai Said Rufai
Mhe. Salim Abdalla Hamad
Mhe. Marina Joel Thomas
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Asaa Othman Hamad
Mhe. Jaku Hashim Ayoub
Mhe. Salmin Awadh Salmin
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Suleimna Hemed Khamis
Mhe. Nassor Ahmed Mazrui
Mhe. Mohammed Said Mohammed

Mhe. Mwenyekiti, Wajumbe waliochangia kwa maandishi ni kama wafuatao:-
Mhe. Asha Abdu Haji
Mhe. Farida Amour Mohammed
Mhe. Viwe Khamis Abdalla
Mhe. Suleiman Hemed Khamis
Mhe. Salma Mohammed Ali
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Salma Mussa Bilali. Huyu yeye alinileta mchango wake asubuhi hii, lakini na yeye yumo kwenye orodha.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwamba michango, maelekezo, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa au waliyotupa tumeyapokea na tutayafanyia kazi ipasavyo kwani yatatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu ili kukidhi matakwa ya wadau wote wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi hapa nchini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwashukuru Wajumbe Baraza lako Tukufu sasa naomba niainishe maeneo yaliyochangiwa kwa ujumla kama ifuatavyo:-

Kwanza ilikuwa uagizishwaji wa minofu ya kuku kutoka Brazil. Nyumba na mashamba ya wizara, mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe pamoja na mradi wa *millennium* MACEMP. Uhaba wa wataalamu na vitendea kazi, mapato, uhaba wa malisho, upandishwaji wa ng'ombe kwa sindano, karantini ya mifugo, taratibu za ukaguzi, uchinjaji wa mifugo na ukaguzi wa mabucha ya kuuzia nyama. Sheria ya Uvuvi namba 7 ya mwaka 2010, soko la Tumbe, Mabwawa na ufugaji wa samaki, uchafu wa soko la samaki la Malindi. Bei

na soko la Mwani, ufinyu wa bajeti ya wizara, Mikopo nafuu kwa wafugaji, uvuvi wa bahari kuu, maeneo ya uhifadhi.

Mhe, Mwenyekiti, sasa naomba kuchukua nafasi hii kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wajumbe pamoja na kuwasilisha majibu kwa hoja zilizotolewa kama ifuatavyo:-

Kwanza nianze na Mhe. Ali Salum Haji Mwakilishi wa Kwahani ambaye alitoa hoja hapa uingizwaji wa minofu ya kuku. Hii dhamira ya ufugaji kuku itapatikana na wizara imejipangaje na ushindani huu wa kibiashara?

Jibu ni kwamba uingizaji wa minofu natumai Mhe. Waziri wa Biashara ameeleza kwa ufasaha na kwa utaalamu wa hali ya juu. Kwa hivyo, mimi nitaeleza tu kwa juu juu kwa sababu Mhe. Waziri ameenda ndani kabisa. Namshukuru sana kwa hilo na imani yangu Wajumbe wameelewa kwa kina.

Kwa hivyo, hii ni biashara huru kama biashara nyengine zinavyoingizwa hapa nchini. Wizara inakiri kwamba biashara hiyo ni changamoto katika maendeleo ya ufugaji wa kuku nchini mwetu. Kwa kulitambua hilo wizara imeandaa mpango maalum wa kuendeleza ufugaji wa kuku nchini. Na kati ya mikakati hiyo ni kuiomba Serikali kutoa fidia kwa wafugaji wa kuku katika chakula na madawa. Hili litapunguza gharama za uzalishaji na kushajihisha ufugaji wa kuku nchini.

Labda nieleze tu kwamba kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe lazima tuwe wakweli na suala hili la kuku, na nimefurahi kwamba Mhe. Salmin Awadh alieleza kwa ufasaha na yeye kasema kufanya *study* na ndio ukweli ulivyo. Lazima tuwe wakweli Mheshimiwa kaeleza katoa kiasi gani cha mahitaji ya kuku nchini na uwezo wetu wa kuzalisha uko vipi. Kwa hivyo, utakuta alaakulli haali ni kwamba lazima tutahitaji kuagizia kuku kutoka nje, hatuna jinsi. Hii ni sawa sawa na mpunga, tunazalisha mpunga hapa lakini bado tunaagizia mchele kutoka nje.

Kwa nini? Kwa sababu kima ambacho tunazalisha hakikidhi. Kwa hivyo, na suala la kuku halkadhalika kadri ya sekta ya utalii inavyokuwa basi na mahitaji ya kuku yanakuwa. Kwa hivyo, kubwa cha kufanya sio kuzuia biashara ambayo iko huru kwa mujibu wa sheria na Mhe. Waziri wa Biashara kaeleza kwa ufasaha kabisa itakuwa tunavunja sheria. Kufanya sisi ni kushajihisha wafugaji wetu na tumo katika hatua hii ya kuwashajihisha wafugaji kuku wetu ili waweze kushindana na kuku kutoka nje, kiutalaamu, mbegu nzuri na tunashukuru kwamba tunaendelea uzuri.

Kwa hivyo, hili suala la kusimamisha ghafla si rahisi, ni lazima linahitaji matayarisho. Kwa hivyo, tumo katika hatua hiyo ya kuwashajihisha wafugaji wetu ili wazalishe kuku bora na kwa wingi. Suala sio kima lakini na ubora vile vile wa kuku. Alisema Mhe. Waziri wa Biashara hapa kwamba tusiwatetee hawa wazalishaji tuangalie na walaji kuku. Lazima niseme ukweli huo.

Kwa hivyo, hatua ya kutoagizishia bado nafikiri tungechukua muda tuwe na subra tuwe na taratibu twende taratibu mpaka tufikie kiwango ambacho wazalishaji wetu watafikia kiwango cha uzalishaji wa kuku na ubora wa kuku. Hapo sasa unaweza kumzuia. Lakini kwa njia ghafla na jazba ngonja tunaweza kuzuia halafu matokeo yake sekta ya utalii bado inahitaji mahitaji ya kuku, na matokeo yake itabidi turejeshe kule kule. Tuagizishie kutoka Bara lazima itakuwa hivyo kwa sababu hatuna uzalishaji mkubwa wa kuku. Kama tunavyofanya mpunga basi na kuku hivyo hivyo. La si hivyo basi tuzuie na mpunga kwa sababu tunazalisha lakini je, unakidhi? Haukidhi.

Kwa hivyo, lazima suala hili tuwe wakweli jamani, sababu za kitaalamu zimetolewa nashukuru Mhe. Salmin Awadh alisema hapa na Mhe. Waziri wa Biashara kaeleza. Waheshimiwa Wajumbe ujumbe umefika na nimeufahamu vya kutosha.
Twende kwenye mradi wa kopa ng'ombe lipa ng'ombe umefikia wapi. Mradi huu bado unaendelea katika mfumo wa skuli za wafugaji nchini chini ya uliokuwa mradi wa *PADEP* na mradi wa *ASPL*. Wafugaji waliopata ng'ombe katika mradi wa kopa ng’ombe lipa ng’ombe walianzisha skuli za wafugaji kuwa wafugaji hao kupatiwa mafunzo ya ufugaji, na hapana shaka ng’ombe wa mwanzo wamezaliwa.

Soko la Tumbe halina ubora na kwamba wananchi wanadai kampuni iliyojenga wizara imechukua hatua gani. Wizara imekutana na kampuni ya ujenzi ndogo na mshauri wa ujenzi huo kwa pamoja wamekubaliana kwamba mkandarasi atafanya marekebisho na iwapo atashindwa kufanya marekebisho ifikapo Agosti 2013 wizara itachukua hatua ya kuzuia *guarantee* ya Benki aliyoiweka ili fedha hizo zitumike kufanya marekebisho yanayohitajika.

Kuhusu madeni anayodaiwa Mkandarasi na wananchi wizara inawashauri kufikisha malalamiko yao katika vyombo vya sheria kwa sababu huu ulikuwa mkataba baina ya Kampuni na wananchi wenyewe, wizara imeshirikishwa. Lakini kwa sababu ni wadau wetu ni wajibu na suala hili tutalichukulia hatua.

Halafu Mhe Salim Abdalla Hamad aliulizia wizara za Mazizini, Chumbuni zinakaliwa na watu ambao si wafanyakazi na uvamizi wa mashamba ya Serikali na hati miliki. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli nyumba zilizojengwa na

Idara ya Maendeleo ya Uvuvi zina madhumuni zilipewa waliokuwa wafanyakazi wa iliyokuwa Wizara ya Kilimo na Maliasili na Mazingira na watu hawa sio wafanyakazi tena wizara. Hivyo yangu nimewataka waliopewa nyumba hizo wahame na kuzirejesha ili zitumiwe na wafanyakazi waliotoka hapa.

Watu watatu wanaoishi ndani ya nyumba hizi wamejibu kwamba wapo tayari kuhama, lakini wametuomba tuwape muda na wizara imetoa muda lakini bado hawajahama. Hivyo wizara imetoa taarifa Mazizini ili kuwachukulia hatua na kuwahamisha kwa utaratibu au taratibu za kisheria.

Nyumba za Chumbuni sasa ziko katika hali ya uchakavu na hakuna mtu anayeishi. Wizara inapanga kutengeneza ili wakae wafanyakazi wake nyumba nyengine zote zilizobaki hivi sasa wanakaa wafanyakazi wetu.

Kuhusu uvamizi wa mashamba ya Serikali wizara imekwisha yapima maeneo yake yote na imetenga fedha za kupatiwa hati miliki. Shamba la Tunguu limechukuliwa na Serikali Wizara ya Ardhi, Makaazi Maji na Nishati na maeneo yake kutolewa kwa taasisi tafauti na Serikali na watu binaafsi.

Shamba la Kisakasaka limekwishapimwa na hati miliki imeshalipiwa. Kwa eneo la Kitumba wizara inaendelea kujadiliana na JWTZ Makao Makuu ya Brigedia ya Nyuki ya Zanzibar waliovamia eneo hilo kuondoka.

Vile vile Mhe. Asha Bakari Makame naye alikuja na hoja Serikali isiruhusu uagiziaji wa kuku. Natumai suala limeelezwa vya kutosha sina haja ya kujibu. Suala hili jibu lake ni kama ilivyoelezwa hapo.

Nyumba za Serikali zimechukuliwa kwa kusingizia ruhusa inatolewa na Mhe. Rais. Muongozo wa kuzidhibiti nyumba za Serikali na kuzifanyia ukarabati umefika wapi? Mhe. Mwenyekiti, jibu lake nimelieleza kwenye hoja ya Mhe. Ali Salum Haji pamoja na ufinyu wa bajeti wizara imekwisha kuzitengeneza nyumba za Mkwajuni, nyumba mbili za Mtoni, nyumba ya Matemwe na Potoa Ofisi ya Dunga, Maabara ya Maruhubi, Ofisi ya Mangapwani, nyumba ya Mtambile, Ofisi ya Chamanangwe, vituo vya Konde, Kengeja, Maabara za Wete na Chake Chake ambazo zipo katika hali nzuri hivi sasa nyumba na ofisi nyengine zinatengenezwa kadri ya hali ya fedha itakaporuhusu.

Mjumbe mwengine aliyechangia alikuwa ni Subeit Khamis Faki alitoa hoja kwamba Serikali iwasaidie wakulima kupata soko la mwani. Kwani mwani uko mwingi majumbani haujanunuliwa. Natumai na suala hili Mhe. Waziri alieleza kwa ufasaha sana kitaalamu kabisa, na hivi sasa hao wanunuzi wa

huo mwani wenyewe basi uko hapa na imani yangu tutafikia pahala muafaka kabisa. Kwa hivyo, kubwa kuwa na subra, kheri kubwa itapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwa Pemba zilitengwa pesa kwa kuwasomesha wafanyakazi, lakini wafanyakazi hawakwenda kusoma. Wizara ina mpango gani kuwasomesha wafanyakazi wake. Jumla ya shilingi milioni tano zimepatikana na kusomesha mfanyakazi mmoja katika fani ya maabara.

Chuo Kikuu cha Sokoine Morogoro kwa mwaka huu wa fedha tunaendelea kuwalipia wanafunzi wengine wawili. Aidha mafunzo mengine mafupi yatatolewa kwa wafanyakazi wengine 24.

Kuhusu vituo havina *furniture* na mabango. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kituo cha Micheweni hivi sasa hakina samani za kutosha. Hii inatokana na uhaba wa fedha tunazopata katika bajeti. Kwanza tulijikita katika ujenzi wa kituo na baada ya ujenzi tutaelekeza nguvu zetu katika kununua nyenzo za kufanyia kazi. Fedha zimetengwa katika bajeti hii kwa ununuzi wa *furniture* za vituo ikiwemo kituo cha Micheweni pamoja na mabango.

Alitoa hoja nyengine kwamba wafugaji wa samaki wapatiwe nyenzo na taaluma. Wizara yangu inatoa nyenzo na taaluma kwa wafugaji wa samaki kwa mujibu wa hali ya bajeti. Kwa mwaka 2012/2013 wizara yangu ilitoa taaluma pamoja na vifaa mbali mbali ikiwemo nyavu kwa vikundi vya ufugaji, majongoo kwa wafugaji wa Matemwe, Mtambwe Kaskazini na Wambaa.

Aidha mabwawa ya mfano yamejegwa na kukabidhiwa wafugaji samaki wa Pujini, Kiungoni na Jozani. Misaada ya nyenzo imetolewa ikiwemo *pump* 4 za kuingiza maji katika mabwawa kwa vikundi vya Chokochoko, Mtangani, Gando na Jozani. Vikundi vya Kokota na Makangale vimepatiwa vifaa vya kulimia mwani ambavyo ni kamba na taitai. Wizara yangu itaendelea na kutoa taaluma za vifaa katika bajeti ya mwaka huu. Uzalishaji wa Chumvi unasimamiwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili elewa hilo.

Hoja nyengine ilikuwa ni uvuvi wa bahari kuu umekuwa ni wa nadharia tu sio wa vitendo. Wizara yangu tayari imetangaza zabuni na kampuni ya Anzai ya Kunduchi Dar -es Salaam na imepata zabuni hiyo. Hata hivyo, kutokana na bei kutoonekana ni ghali sana. Wizara imeshauriwa na Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo kutangaza tena zabuni hiyo kwa njia ya mchujo. Hivi sasa tuko katika mchakato huo wa mchujo. Boti itakayonunuliwa itatumika kwa mafunzo ya vitendo kwa wavuvi ili kuwawezesha kuvua katika bahari kuu.

Hoja nyengine ilikuwa ni soko la Samaki Malindi ni chafu na mazingira hayaridhishi. Usafi wa soko la samaki Malindi unasimamiwa na Baraza la Manispaa elewa hilo. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwa Baraza lako tukufu kuwa kuanzia mwaka jana Novemba walikuja washirika wa kimaendeleo *JICA* kufanya *feasibility study* hatua ya kwanza mwaka huu, na pia Juni mpaka Julai mwaka 2013 watafanya hatua ya pili.

Tunategemea mwezi wa 8 watachora mchoro wa soko la kisasa na diko ili kujenga soko kama la Feri Dar- es Salam kwenye eneo la Malindi ili kuboresha samaki na sehemu ya kushushia samaki. Mradi huu unategemea kupitishwa na *cabinet* ya Japan mwaka huu. Tukijaaliwa soko hilo ujenzi utaanza Julai 2014 na kampuni kutoka Japan. Ujenzi huu unategemea kukamilika mwaka 2015.

Mhe. Hassan Hamad Omar alikuja na hoja zake na yeye ufugaji wa samaki mafanikio yake bado hayajaonekanwa. Mhe. Mwenyekiti, ufugaji wa samaki umepata mafanikio makubwa katika mwaka 2012 jumla ya tani 9.8 za samaki zimenunuliwa katika mabwawa ya samaki Unguja na Pemba. Pamoja na mafanikio haya wizara yangu inaendelea kufanya tathmini ya kuona vikwazo vinavyoathiri mafanikio ya uzalishaji ili kupatiwa ufumbuzi.

Aidha namuahidi Mhe. Hassan Hamad Omar kuwa tutashirikiana naye na katika kutembelea wafugaji wa samaki katika Jimbo lake ili kuendeleza wafugaji wa samaki na kukabiliana na changamoto zinazowakabili. Alikuja na hoja nyengine kwamba mwani ni kazi ambayo inafanywa kwa asilimia kubwa na wananchi walio wengi na vijiji vya Zanzibar. Lakini jambo la kusikitisha ni kwamba mwani huo hauna thamani hata kidogo kazi ya mwani ni ngumu.

Natumai tumeeleza hayo Mhe. Waziri wa Biashara ameeleza kwa kina. Kwa hivyo, natumai ujumbe umefika. Mhe. Mwenyekiti, tujenge subira kidogo na tutaona hatma yake. Vile vile hoja ya sheria namba 7 ya mwaka 2010 imezuia matumizi ya vioo na gesi kwa wavuvi tatizo la gesi na vioo ni nini.

Sheria namba 7 ya 2010 Mhe. Hassan Hamad Omar imezuia matumizi ya zana za kuzamia za gesi na vioo kwa shughuli za uvuvi kwa sababu zifuatazo:

- Wavuvi wengi sana wa Zanzibar walipendekeza kuzuia kwa zana hizo wakati wa mchakato wa kutengeneza sheria hiyo katika mikutano wa kupata maoni ya wadau.
- Zana hizo husababisha uvuvi wa kupindukia na uharibifu mkubwa wa mazingira ya baharini. Zana hizo humuwezesha mtumiaji kukaa chini ya maji na kufanya uharibifu anaotaka. Matumizi ya zana hizo yamesababisha

viumbe wengi kutoa mfano majongoo, bahari, madondo kama kamba wakubwa na jamii yote ya makome.

Aidha kutopea kwa viumbe hawa husababisha mabadiliko ya mfumo wa kimaumbile wa bahari. Ongezeko la viumbe kama mashanuo, wavuvi wanaotumia zana hizo wameshasababisha uharibifu wa matumbawe kwa kutumia nyavu za macho madogo.

Mhe. Ismail Jusa Ladhu na yeye alikuwa na hoja. Ingawaje na yeye vile vile alipata jawabu kutoka kwa Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, labda kwa faida yake tu nimueleze kwamba fedha nyingi zimetumika kununua mali za mradi wa *MACEMP*. Je, kumefanyika uhakiki wa mali hizo zina thamani gani na ziko wapi. Natumaini umejibiwa lakini nitaongeza kwa faida yako na kwa faida ya Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, mali zote za mradi wa *MACEMP* zilikuwa zinahakikiwa kila zilipokuwa zikinunuliwa. Aidha utaratibu wa mradi ni kwamba mali zote kabla ya kununuliwa hufanyiwa tathmini na baada ya kununuliwa huhakikiwa ipasavyo. Mali za mradi hupelekwa katika taasisi mbali mbali ikiwemo Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, Idara ya Mazao ya Baharini ambazo wizara yangu inazisimamia.

Nyengine ni mamlaka ya kusimamia uvuvi wa bahari kuu. Wizara ya Kilimo na Maliasili, Idara ya Nyaraka, Idara ya Ardhi na Mipango, Idara ya Tawala za Mikoa, Kamisheni ya Utalii ambazo taasisi zenyewe ndizo wasimamizi wa mali walizopewa. Mali zote zilikuwa na thamani ya dola za kimarekani hapa sijatoa *figure* lakini natumai Mhe. Naibu Waziri ameieleza.

Hoja ya pili je, *account* ya mradi wa *MACEMP*. Wakati wote wa utekelezaji wa mradi *account* za mradi zilikuwa zikikaguliwa kila baada ya miezi sita na mkaguzi wa ndani na wakaguzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Fedha za makusanyo katika maeneo ya hifadhi ya bahari zinakwenda wapi na kwenye *account* gani. Hadi hivi sasa kuna maeneo matatu ya hifadhi ya bahari. Nazo ni *MBCA*, *MIMCA* na *PECA* fedha zinazokusanywa zinatokana na sheria ndogo ndogo *LN* 43 ya mwaka 1997 kwa hifadhi ya *MBCA*.

Aidha sheria hizi zimetokana na kifungu cha sheria namba 7 na 32 cha sheria mama namba 8 ya mwaka 1988. Kwa hivyo, fedha zote zinazokusanywa asilimia mia hutiwa katika *account* ya maeneo haya ya uhifadhi yaani *MBCA*, *MIMCA* na *PECA;* ambapo mgawanyiko wake ni asilimia 70 hutumiwa kwa ajili ya maeneo hayo na asilimia 30 hutumika kwa hatua za kutatua matatizo ya kijamii yanayoombwa na wavuvi wenyewe kupitia kamati zao. Suala la

kughushi leseni natumai limeelezwa kwa ufasaha mkubwa namshukuru Mhe. Naibu Waziri na nimpe hongera sana ndugu Zahor nafikiri sina haja tena kutoa namba ya ardhi. Lakini twende moja kwa moja kwenye hoja nyengine ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu, makisio ya makusanyo ya bahari kuu ni umeelezwa vile vile ni bilioni mbili milioni sabini na saba. Lakini mapato halisi ni kidogo yaani kama yalivyoelezwa na Mhe. Naibu Waziri ni milioni mia moja na arubaini na sita na lakini tano na sitini elfu.

Mhe. Mwenyekiti, makisio haya ya bilioni mbili ni makisio yalipangiwa kukusanywa na Serikali zetu mbili yaani SMT na SMZ kwa mwaka wa fedha 2012/2013. Na hadi mwezi Juni 2013 Mamlaka imekusanya bilioni hizo mbili ambazo ni zaidi ya makisio kwa shilingi 87 milioni.

Mgao wa SMZ kutoka kwenye mkusanyo huo ni kama ulivyoelezwa hapo ni shilingi milioni mia nne na thalathini na mbili na ushee sawa na asilimia 20 ya makusanyo yote na shilingi mia moja arubaini na sita na ushee hizo zilizoandikwa kitabuni ni fungu la SMZ hadi mwezi wa Aprili 2013 wakati bado makusanyo ya mwezi wa Mei na Juni yalikuwa hayajakusanywa. Kwa hivyo, mtiririko ni kama ufuatavyo.

Mchangiaji mwengine alikuwa ni Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwa nini wizara haitengi eneo maalumu la malisho ili kulisha mifugo yetu wakati wa kiangazi. Ushauri wa Mheshimiwa Mjumbe ni mzuri lakini unahitaji maamuzi ya taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Ardhi Makaazi, Maji na Nishati ambao ndio yenye ardhi.

Hoja ya pili ilikuwa ni kwa nini tuna uhaba wa wataalamu wakati wapo vijana wengi waliosoma. Jawabu ni kwamba Mhe. Mwenyekiti, kuna uhaba wa watalaamu wa uvuvi na mifugo kulingana na mahitaji ya wizara yangu ya kuwapatia huduma wafugaji na wavuvi. Lengo letu ni kuwa na wataalamu katika kila shehia uajiri wa wataalamu kunatumia uwezo wa Serikali vile vile.

Hoja ya tatu kwa nini tumejenga mitambo ya *biogas* kufikia 24 wakati tukiwa na uhaba wa wataalamu. Jawabu ni kwamba uhaba wa wataalamu uliokuwepo kwenye sekta ya mifugo hauathiri ujenzi wala uendeshaji wa mitambo ya *biogas*. Uhaba wa wataalamu tuliokuwa nao katika utabibu na uzalishaji wa mifugo na sio katika uendeshaji wa mitambo ya *biogas*. Mitambo hii tuliendesha wenyewe, na huhitaji taaluma ndogo ambayo hata mfugaji mwenywe anaweza kufundishwa namna ya kusimamia.

Hoja yake ya nne ilikuwa. Je, wajasiriamali wanaopelekwa China mafunzo wanayoyapata yanawasaidia kwa kuyatumia. Wajasiriamali waliopata mafunzo China wameweza kutumia taaluma hiyo kuongeza uzalishaji katika

mabwawa yao; Mfano kikundi cha Mtambwe Kaskazini ambao kabla walikuwa wakifuga samaki tu. Lakini baada ya kupata mafunzo China wameongeza ufugaji wa mazao mengine kama kaa na majongoo.

Pia wako walioboresha ujenzi wa mabwawa ya ufugaji wa samaki kama vile kikundi cha Leo ni leo cha Jadida Wete na Pujini. Wajasiriamali wengine wamejiendeleza katika ufugaji wa kasa kwa shughuli za utalii na kujiongezea mapato Nungwi na Jozani.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa naye aliuliza hoja hiyo mradi wa *MACEMP* umefikia hatua gani. Mradi wa *MACEMP* umemalizika tangu tarehe 15/2/2013. Hoja yake nyengine zoezi la kufungwa uzazi kwa paka na mbwa, kuchanja dhidi ya kichaa cha mbwa limefikia wapi?

Zoezi la kuhasi wanyama; paka na mbwa bado linaendelea chini ya mradi wa *WSPA* ikishirikiana na serikali. Zoezi hili hufanyika kituo cha Maruhubi, mwaka huu wa 2013/2014 zoezi hili litafanyika katika vituo vya wilayani. Pia zoezi la kudhibiti kichaa cha mbwa bado linaendelea kwa Unguja na Pemba, hivi sasa idara yangu inafanya tathmini ya idadi ya mbwa na paka ili kupata idadi halisi ya wanyama hawa na kurahisisha mpango wa uchanjaji.

Hoja yake ya tatu ilikuwa ni kutafuta utaratibu wa uchinjaji na ukaguzi wa ng'ombe na mabucha. Mhe. Mwenyekiti, kwa kushirikiana na bodi ya chakula, madawa na vipodozi wizara yangu itatekeleza taratibu za uchinjaji, ukaguzi wa ng'ombe na mabucha na uchunguzi wa maziwa.

Hoja yake ya nne kuwasaidia wafugaji wa kuku taaluma na masoko ili kukabiliana na ushindani. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii nimeshajibu wakati nilipokuwa najibu hoja ya Mhe. Ali Salim hapa. Hoja yake ya hata mwenendo wa upandishaji wa mbuzi kwa njia ya sindano. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu ilitaka kupata taaluma hii kutoka Kenya, lakini walilotupatia ni kwamba wao hawajaanza matumizi hayo kwenye mbuzi. Hivi sasa ndio wanajipanga kuanza na watakapokuwa tayari na wakishabobea ndipo watakapotupa taaluma hiyo.

Mhe. Saleh Nassor Juma na yeye alikuja na hoja ya kupatiwa msaada wazalishaji wa lulu Wilaya ya Mkoani na kupatiwa elimu wafugaji wa samaki Vitongoji. Mhe. Mwenyekiti, bajeti iliyopita wazalishaji lulu wa Makombeni na Michenzani walipatiwa mafunzo na taaluma kutoka Unguja. Katiba bajeti ya mwaka huu pia tunatenga fedha ya kuwapatia vifaa vya usarifu wa lulu, makombe na mafunzo ya usarifu. Namuahidi Mhe. Mwakilishi kwamba tutawatembelea wafugaji wa samaki Vitongoji na kuwapatia taaluma ili kuboresha uzalishaji.

Hoja yake nyengine ni kwamba nini hatima ya mashamba ya Mkakata na Chamanangwe. Mhe. Mwenyekiti, baada ya serikali kujitoa katika uzalishaji shamba la Mkakata lilikodishwa kwa Shirika la Biashara *ZTC* kwa ajili ya Kiwanda cha Makonyo. Shamba la Chamanangwe bado liko mikononi mwetu na linaendeshwa kama kituo cha utafiti cha mifugo. Kwa mwaka huu wa fedha wizara itafanya michoro ya majengo pamoja na ujenzi wa kituo kidogo cha utafiti wa kuku.

Hoja yake nyengine ni kuhusu ushauri wa kuyafufua majosho ya ng'ombe. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu imo katika jitihada ya kuyafufua majosho kwa mujibu wa bajeti inavyoruhusu. Kwa kuanzia josho la Makangale Pemba na josho la Binguni Unguja yameanza kufanyiwa ukarabati.

Mhe. Asha Abdu Haji na yeye alikuwa na hoja ya kuhusu dawa ya chakula cha mifugo ni ghali, hivyo serikali ipunguze ushuru wa bidhaa hizo. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inaandaa waraka wa kupeleka serikalini kwa kuondoa au kuomba fidia katika madawa ya chakula cha mifugo, ili kuweza kumudu ushindani wa bidhaa za mifugo kutoka nje.

Vile vile kuhusu wizara ishajihishe wananchi kuwapa ng'ombe wengi ili wapate mbolea nyingi na waweze kujenga mitambo mingi. Mhe. Mwenyekiti, wizara imechukua ushauri huo na itaendelea kushajihisha wafugaji wenyewe ili waweze kujenga mitambo mingi na kuweza kuwapatia nishati mbadala.

Hoja yake nyengine ilikuwa ni kuwawezesha kitaaluma na nyenzo wafugaji wa samaki. Migogoro ya maeneo na wawekezaji mahoteli, bei ndogo ya mwani. Natumai hayo yameelezwa vizuri. Ni kwamba wizara yangu inawezesha kwa kadiri inavyowezekana wafugaji wa samami. Kwa mfano wafugaji wa samaki kutoka Shungi Makunduchi, Bumbwini na Uzi walipelekwa Pemba kujifunza na kuona ufugaji katika mabwawa ya mfano. Pia waliporudi Unguja walipatiwa mafunzo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu migogoro ya maeneo na wenye mahoteli, wizara yangu itashirikiana na taasisi zote zinazohusika na utalii, uwekezaji, ardhi na upimaji na wadau wengine ili kuona wavuvi na wakulima wa mwani wanaendesha shughuli zao bila ya shida au kuzibiwa njia za kuelekea pwani.

Mhe. Mwenyekiti, suala la bei ya mwani nimeshalitolea maelezo kabla. Hoja nyengine ya ufugaji wa kuku ni mgumu na ghali, kwa ughali wa chakula, madawa pamoja na uingizaji wa kuku kutoka nje. Hayo yameelezwa nafikiri. Kuhusu wavuvi kusalimisha nyavu zisizofaa ili wapewe nyavu zinazofaa.

Wavuvi wote ambao walisalimisha nyavu zao waliweza kupewa nyavu nyengine kwa shughuli zao za uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Farida Amour Mohammed na yeye alikuja na hoja ya kwamba ni lini wizara itajipanga vizuri kusaidia wafugaji wa mazao ya baharini, kilimo na misaada mingine. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii nimeshajibu wakati najibu hoja ya Mhe. Subeit Khamis Faki.

Vile vile Chamanangwe kuna eneo kubwa lakini limetupwa ni lini litafufuliwa pamoja na kituo cha Ole. Mhe. Mwenyekiti, hoja ya shamba la Chamanangwe nimeshalijibu wakati nilipokuwa natoa ufafanuzi kwa hoja ya Mhe. Saleh Nassor Juma.

Kituo cha Ole vile vile kinatarajiwa kufanyiwa ukarabati na mradi wa *MIRVAF* ili kuwa ni Chuo cha kufundishia usarifu wa mazao ya mifugo kama siagi, samli, jibini na mtindi. Kuhusu wizara imejipanga vipi kufanya tathmini na kujua ni vikundi vingapi vya ufugaji kuku vipo katika kila Shehia na vipi wizara itavisaidia kwa taaluma. Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu inavitambua vikundi vyote vya ufugaji kuku kwa Unguja na Pemba ambavyo vimeanzishwa kisheria na kuna utaratibu wa kuwatembelea ili kujua changamoto na kuwapatia taaluma ya kuzitatua.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa swali lake kwa nini mapato kwa wizara yameshuka. Mhe. Mwenyekiti, lengo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ni kwamba karibu mara mbili kuliko lengo la mwaka 2011/2012, kutokana na ukubwa wa ongezeko la lengo la kukusanya mapato na uwezo wa vyanzo vyetu vya mapato kuwa finyu hatukuweza kufikia lengo hilo. Pia bajeti ndogo ya wizara na uhaba wa wafanyakazi umechangia kupungua kwa ukusanyaji wa mapato.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yake ya pili kwa nini pawepo na kasma za matengenezo madogo nafikiri alijibiwa na matengenezo makubwa wakati jengo la wizara ni jipya. Mhe. Naibu Waziri alijibu, lakini kwa faida yake. Ujenzi wa jengo letu jipya la Nyangumi, hapakuwepo kipengele cha ujenzi wa uzio. Kwa hivyo, wizara imeamua kujenga ukuta huo kwa awamu na kwa kutumia mafundi wake. Kwa hivyo huo ujenzi mkubwa ulioainishwa hapo ni ujenzi wa ukuta wa ofisi ya wizara.

Hoja yake ya tatu ni kuhusu fedha za makusanyo za maeneo ya hifadhi na mgawanyo wake kwa kipindi cha miaka miwili. Jibu ni kwamba hoja hii niliijibu wakati nilipokuwa nikimjibu Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Mhe. Rufai Said Rufai na yeye alikuja na hoja zake kuhusu vifo vya ng'ombe wa maziwa. Ili ufugaji uwe endelevu na wenye tija ni lazima mfugaji afuate masharti ya ufugaji bora, kama vile majani ya kutosha, kukogeshwa, dawa ya minyoo, chanjo, kupata matibabu mapema na pia mfugaji kuwa na shauku kubwa na kufuata maelekezo ya mara kwa mara kutoka kwa wataalamu wa mifugo.

Mhe. Mwenyekiti, wafugaji ambao wanafanikiwa ni wale ambao wanafuata masharti niliyoyataja hapo juu. Wizara yangu inaendelea na jitihada za kutoa taaluma kwa wafugaji ili ufugaji wao uwe na tija zaidi. Tunatumia njia mbali mbali za kufundishia; kama majarida, TV na redio, kuwatembelea wafugaji na kuwapatia ushauri na misaada mbali mbali. Wafugaji wanaofuata ushauri wanafanikiwa na mifugo yao huwa na tija na kuishi muda mrefu.

Vile vile soko la Tumbe haliko katika hali inayoridhisha na kampuni pia haina kiwango. Mhe. Mwenyekiti, hili pia nimelijibu nilipokuwa najibu hoja ya Mhe. Ali Salum Haji. Pia Mhe Salim Abdalla Hamad na yeye alitoa hoja nafikiri nazo nimezijibu.

Mhe. Marina Joel Thomas. Je imefuatiliwa na kuona mafanikio na kama kuna mabadiliko baada ya wajasiri amali kupatiwa mafunzo ya ufugaji wa mazao ya baharini. Hoja hii nimeshaijibu wakati nilipokuwa najibu hoja ya Mhe. Hassan Hamad Omar. Hoja yake ya pili, je wizara imefanya utatifi wowote kuhusu mahitaji ya soko la ndani. Ndio wizara imefanya utafiti wa mizani juu ya mahitaji ya nyama ya kuku nchini na tuligundua kuwa tunahitaji jumla ya tani 7 kwa mwaka. Nafikiri imeelezewa vizuri sana na Mhe. Nassor Ahmed Mazrui Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, wakati uzalishaji wa ndani ni tani 1,950 hivyo kuna mapungufu ya kama tani 4 hivi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk hoja yake nafikiri nimeshajibu. Mhe. Asaa Othman Hamad na yeye alijibiwa. Iwapo kama soko la Tumbe limeshakabidhiwa au la, wizara imechukua hatua gani. Mhe. Mwenyekiti, soko Tumbe limekabidhiwa na hoja hii nimeshaitolea maelezo nilipokuwa najibu hoja ya Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuhusu Kiwanda cha Kusindika Samaki. Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa hadi hivi sasa hakuna kiwanda cha kusindika samaki hapa Zanzibar, hii inatokana na kwamba kiwango cha samaki kinachovuliwa kinatosheleza mahitaji ya ndani tu. Hata hivyo, juhudi za kuongeza uzalishaji wa samaki kwa kuendeleza uvuvi katika bahari kuu zinafanyika, kuongezeka kwa uzalishaji na upatikanaji wa samaki wa ziada kutawezesha kuanzisha viwanda vya kusindikia samaki na kusafirisha nje ya nchi.

Halikadhalika Mhe. Salmin Awadh Salmin na yeye vile vile alikuwa na hoja kuwa Je, wizara ina madaktari wa mifugo wangapi na upungufu wa vifaa vya matibabu? Mhe. Mwenyekiti, wapo madaktari wenye Shahada ya Chuo Kikuu watano tu, na wengine waliobakia ni vijana wenye diploma, vyeti na wahudumu. Upungufu wa vifaa vya huduma za utabibu wa mifugo bado ni mkubwa, zikiwemo darubini, vifaa vya maabara, madawa na usafiri. Vifaa hivi na madawa ni ghali lakini hata hivyo wizara yangu inavinunua kwa mujibu wa bajeti yetu.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yake nyengine ni kuhusu wajasiri amali wa sekta ya mifugo wamelaghaiwa na kunyang'anywa fedha zao baada ya kuahidiwa kupatiwa mifugo na mtu aliyeshirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wilaya ya Kusini na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Samahani.

Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu haijashirikishwa wakati wa kumkaribisha Mjasiri amali huyo. Wizara imepata habari ya tatizo hili baada ya wajasiri amali hao kunyang'anywa fedha zao. Tumelifuatilia suala hili kwa nia ya kuwasaidia wajasiri amali hao wa mifugo, lakini sisi hatuna nguvu ya kisheria kumchukulia muhalifu yeyote aliyefanya hayo kwa vile hatuna mikataba ya wajasiri amali hao au muhusika wa ulaghai huo. Wizara inashauri wajasiri amali hao walioathirika basi wafungue mashtaka na wizara itawasaidia. Mhe. Mwenyekiti, kufuatia kadhia hiyo wizara yangu inawaomba wafugaji wawasiliane na wizara kabla ya kuingia mikataba na watu wa aina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yake ya tatu kama vifaa vya *MACEMP* vimefanyiwa tathmini, na kwa nini mradi huu haukutengewa fedha za kuendeleza kazi. Mhe. Mwenyekiti, ufafanuzi wa hoja hii tayari nimeshautoa nilipokuwa najibu hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Vile vile Mhe. Viwe Khamis Abdalla, aliuliza mbuzi wa maziwa ni muhimu katika kuendeleza wananchi hasa walioko vijijini, kutokana na soko na uzuri wa maziwa ya mbuzi pamoja na mbuzi wenyewe. Wizara ilitoa elimu maalum kushajihisha wananchi kufuga mbuzi wa maziwa, pamoja na mikakati madhubuti ya upatikanaji mzuri wa maziwa. Mhe. Mwenyekiti, napenda kukubaliana na hoja ya Mhe. Viwe Khamis Abdalla, kuhusu umuhimu wa ufugaji wa mbuzi wa maziwa na ubora wa maziwa ya mbuzi.

Pia ningependa kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba tutatembelea kushajihisha wananchi kufuga mbuzi wa maziwa, pamoja na kutoa taaluma ya ufugaji wa mifugo mingine kwa kutumia njia mbali mbali zikiwemo kuwapitia wafugaji kwenye maeneo yao, kutayarisha vipindi vya TV na redio, vipeperushi, mikutano na mafunzo ya vikundi na kadhalika.

Hoja yake nyengine ni kuhusu matayarisho ya ujenzi wa kiwanda cha mwani Tumbe Pemba yamefikia wapi kwa kushirikiana na Korea. Eneo la ujenzi wa kiwanda cha mwani Tumbe lilipimwa, na kuwekewa alama yaani *beacon.* Kwa sasa kinachosubiriwa ni kupatiwa hati miliki na kusainiwa kwa makubaliano ya ujenzi wa kiwanda cha usarifu wa mwani.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis, hoja yake kuhusu kutoa kipaumbele kwa mifugo ya asili. Namshukuru Mhe. Mjumbe kwa mapendekezo yake na wizara yangu itafanya kazi na upande wa uzalishaji pumba, wizara yangu na wizara ya fedha itafanya mazungumzo na Bakhressa juu ya uzalishaji wa kampuni ya maziwa na ambapo itatoa huduma ya pumba kwa wafugaji watakaomuuzia maziwa katika kampuni yake.

Vile vile wazalishaji wa mwani wanawake wasaidiwe nyenzo na wawatembelee. Mhe. Mwenyekiti, hoja hii nimeshaitolea maelezo nilipokuwa najibu hoja ya Mhe. Subeit Khamis Faki.

Mhe. Hija Hassan Hija, hoja yake kwamba kwa nini wizara inakuwa nzito kudhibiti uharamia na wizi wa meli za kigeni. Jibu ni kwamba wizara yangu inafanya jitihada kubwa katika kudhibiti uharamia wa wizi wa meli za uvuvi kwa kushirikiana na mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu, takriban sasa ni zaidi ya miaka mitano hatujaweza kukamata wala kuona meli za uvuvi zikivua kiharamia. Mhe. Mwenyekiti, doria za pamoja hufanywa ambazo zinawashirikisha wavuvi wa KMKM, JSFA, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu na Idara ya Maendeleo ya Uvuvi ikiwa ni pamoja na doria za ndege saba na za baharini tatu. Meli za mizigo na utafiti zilikutikana baharini zikiwepo kihalali nchini. Aidha, meli moja ilikamatwa na samaki na kupelekwa Tanzania Bara na kuhukumiwa.

Mhe. Abdi Mossi Kombo wa Jimbo la Matemwe, hoja yake kwamba nchi yetu inazungukwa na bahari lakini bado wavuvi wako hali duni na serikali bado haijawafikiria wavuvi wa Unguja na Pemba, serikali ijiandae kuhakikisha wanapatiwa vyombo vya kisasa kuliko kuwakandamiza kwenye kuvua. Jibu ni kwamba tunapenda kumjulisha Mhe. Mwakilishi kwamba serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kuwaendeleza wavuvi wa visiwa hivi na lengo ni kuwaendeleza. Aidha, serikali kwa kupitia wizara yangu imechukua hatua za makusudi za kuwapatia vifaa, nyenzo mbali mbali pamoja na vyombo vinavyohitajika kwa uvuvi wa kienyeji, kwa kupitia mradi wa *MACEMP* kutoka mwaka 2005 hadi mwaka 2012. Lakini pia nakubali kwamba vifaa hivyo havijatosheleza mahitaji, na serikali inaendelea na kutafuta uwezekano wa kuweza kuwasaidia wavuvi hao.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa ufafanuzi huo, nachukua fursa hii kuwashukuru wale wote waliochangia hoja hii na wale waliotoa ushauri, nawahakikishia kwamba ushauri wao tutauzingatia kwa manufaa ya wadau wote wa sekta ya mifugo na uvuvi. Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, toa hoja.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nimesema, narudia tena Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.
Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja sasa nitawahoji wale wanaokubali hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. Mhe. Waziri rudi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kukubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Sasa naomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kuanza kamati yetu naomba kuzungumza machache. Leo ni siku ya Ijumaa na tunajua kwamba leo ni siku fupi. Kwa hivyo, kutokana na ratiba yetu leo tumalize wizara hii na hivi sasa tuna saa moja na dakika kumi ya kumaliza wizara hii. Tayari Mhe. Waziri wa Biashara, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Waziri wa Mifugo na Uvuvi mwenyewe wameshatoa baadhi ya ufafanuzi ambao unaweza kuturidhisha.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe, naomba sana twende kwenye hoja muhimu na yale mengine ambayo wameyaahidi kuyafanya basi tuwape muda waweze kuyafanya. Kama haitokuwa hivi kumaliza leo, basi tutakwenda kabisa nje ya utaratibu ambao tumeupanga. Kwa hivyo, ningewaomba sana Waheshimiwa Wajumbe, twende katika hoja ambazo zitakuwa zinaweza kusaidia kumaliza leo wizara hii bajeti yake. Nawashukuru sana.

FUNGU 22 - WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Kifungu 0012	Idara ya Mazao ya Baharini Pemba	21,000,000
Kifungu 0014	Idara ya Huduma za Utibabu wa Mifugo Pemba	12,000,000
Kifungu 0015	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba	6,000,000
Kifungu 0016		

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii na nitumie fursa hii kwa sababu ndio nanyanyuka mara ya mwanzo kuwashukuru sana Mhe. Waziri, Naibu Waziri kwa kutuonesha mfano leo kwa jinsi wanavyoweza kuwa wazi katika kutuwekea sawa yale mambo ambayo tunayauliza humu kwa maslahi ya nchi yetu na watu wake, nawashukuru sana kwa hili.

Nawaomba na Mawaziri wa wizara nyengine waige mfano kama huu na kama ule aliouonesha Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji, siku ya mwanzo tulipoibua suala la ufisadi hapa na yeye akashirikiana na sisi kulieleza kinagaubaga. Tukiwa na utendaji kama huu utatusaidia mengi sana katika Baraza hili kuepusha mivutano iliyokuwa haina ulazima baina ya Mawaziri na Wawakilishi ambao sio sehemu ya serikali.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo katika mchango wangu nilichangia suala la mapato yanohusika na mambo mawili katika idara hii. Kwanza ni mapato yanayohusu hizi hifadhi za bahari, ambazo kwa bahati nzuri Mhe. Waziri kazitaja kama ni tatu, na katika kitabu cha Mhe. Waziri katika ukurasa wa 79 zimetajwa pale. Kuna CHABAMCA, TUMCA na KIMCA.

Mhe. Mwenyekiti, nilihoji katika kifungu hiki kwamba kuna ada ya dola 5 ambayo wanatozwa wageni wanapotembelea hifadhi ile, na nikataka kujua mapato haya yanaingia wapi. Katika majibu yake Mhe. Waziri kaniambia kwamba yanaingia katika *account* za hizi Jumuiya na kwamba asilimia 70 inakwenda katika uendeshaji na asilimia 30 inakwenda katika kuhudumia shughuli za kijamii katika maeneo haya.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ufahamu wangu pamoja na kwamba hizi ni taasisi za kijamii, lakini haya mapato ni ya serikali na mimi najua kwamba wao ndani ya wizara wanajua, kwamba suala hili limekuwa mjadala kwao. Sasa hebu atuambie kwamba asilimia 30 kwenye hayo maeneo yanayozungumzwa wananchi wanalalamika hawaipati, hizo jumuiya tatu alizozitaja katika kitabu chake, seuze ile asilimia 70.

Kwa hivyo, hebu Mhe. Waziri atueleze kweli, katika mchango wangu nilizungumza hapa kwamba kuna mtendaji mmoja katika watendaji wao anajifanya mfalme katika wizara hii, ambaye anafikia hata kukaidi maagizo yao wao wakubwa wenzake. Sasa hapa Mhe. Waziri anatujibu kwamba na kiilivyo na kinadharia tuko sahihi, asilimia 70 inakwenda katika uendeshaji labda na asilimia 30 inakwenda katika shughuli za kijamii. Lakini ushahidi kwamba hizi fedha hazifiki kote, ni kuwa mimi nimepata taarifa na hao wenyewe wenye hizi taasisi, hizi asilimia zao hawazipati, seuze hizo asilimia

70. Kwa hivyo, hebu atueleze ukweli katika wizara kuna nini katika idara ya maendeleo ya uvuvi kwenye kifungu hiki.

Lakini cha pili nimalizie Mhe. Mwenyekiti, ili nisisimame mara mbili ni suala la mapato uvuvi wa bahari kuu. Nimeliuliza, lakini hapa nasikitika kusema pamoja na sifa nilizowapa kwamba siridhiki na mchanganuo wa mahesabu yao. Katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri na akaja akathibitisha Mhe. Waziri wamesema kwamba yale makisio ambayo yametajwa mwaka jana ambayo yalikuwemo katika kiambatanisho nambari 11 ya shilingi bilioni 2,077,000,000 na baadae mapato yakawa ni shilingi milioni 146,560,000. Katujibu kwamba shilingi bilioni 2,077,000,000 yalikuwa ni makisio ya mapato ya jumla ya mamlaka na mgao wa Zanzibar ulipaswa kuwa hivyo.

Mimi sikubaliani na maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kwa ilivyo itakuwa jambo la ajabu kubwa kwamba waje watumie katika kitabu chao makisio ya mapato ya Mamlaka nzima wakati wakijua yanayoingia katika hazina ya Zanzibar ni asilimia 20. Mwaka juzi Mhe. Mwenyekiti, nilichangia hapa nikaonesha tofauti ya takwimu za mapato zinazoripotiwa katika Baraza na katika Bunge na jinsi tunavyonyang'anywa mapato yetu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika hesabu. Sasa sitaki kuanzisha hoja mpya, lakini nataka nipate maelezo pale, kwamba kama ni hivyo ilikuaje wakaingiza makisio ya mamlaka wakati wanajua kinachoingia katika hazina ya Zanzibar ni kile kiwango cha Zanzibar, lakini ukilinganisha mtiririko wa mapato ya uvuvi wa bahari kuu yanaonekana kwamba kumekuwa na takwimu zinazopishana baina ya Baraza na Bunge, lakini bado Zanzibar haipati haki yake. Nilisema Mhe. Mwenyekiti, jana kwamba ukiingia katika fedha za maendeleo Serikali ya Zanzibar inatakiwa bado ichangie milioni 100 wakati mapato yake yanakuwa ni milioni mia moja na …

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe nenda katika hoja.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakwenda kwenye hoja Mhe. Mwenyekiti. Nasema ukitizama makusanyo halisi hapa yanaambiwa ni 146 milioni, wakati huku katika mchango wenyewe tunaoneshwa kwamba bado Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itoe milioni 100. Kwa hivyo, bado nataka niwekewe wazi suala la makusanyo ya uvuvi wa bahari kuu na hasa hoja yangu ambayo nasema, kama ikiwa mapato yetu yanashuka, kwa nini tuendelee kubakisha uvuvi wa bahari kuu uendeshaji wake katika Muungano, naomba maelezo Mhe. Mwenyekiti, kwa masuala yote mawili, la bahari kuu na lile la mapato yanayotokana na zile jumuiya. Naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nafikiri tumetoa takwimu hiyo, sasa labda Mhe. Mjumbe hakuridhika nayo, anasema

kwamba kuna baadhi ya wavuvi hawapati mapato hayo. Inawezekana ni kweli na inawezekana sio kweli. Kwa ufupi sisi kama wizara tumeuona udhaifu huo katika sheria yetu na ndio maana hatukujaribu kufanya marekebisho tumeleta kanuni, ili kuona kwamba haya mahesabu yote yawe yanakuja moja kwa moja kwenye wizara, yasibakie kwenye kurugenzi, kwa sababu Waziri hapa ndiye muhusika na kanuni hii ipo kwa Mwanasheria Mkuu nayo tumejaribu kuya-*accommodate* masuala kama haya ili kuona kwamba kuna uwazi katika masuala ya hesabu ili wizara ielewe. Lakini kwa sheria hivi sasa utakuta mapato hayo hatuna ule mkono wa moja kwa moja, kwa sababu sheria imenifunga yako kule kule kwenye masuala ya idara na kamati.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe waelewe kwamba kanuni ipo ambayo inaya- *accommodate* hayo ambayo Mhe. Mjumbe ana wasi wasi nayo. Ni imani yangu ni kwamba wavuvi pamoja na wanakamati wote wawe na subira, kanuni inayokuja kwa kweli itawanufaisha kwa kiasi kikubwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Ni kweli Mhe. Mjumbe ameonesha *concern* yake ya kutaka kujua hii hesabu kamili. Lakini kupanda na kushuka kimapato inatokana na zile meli zenyewe na *season* yenyewe inavyokuja. Kama sasa kuna Somali meli nyingi sasa zinafanya zisije ndio tunashuka mapato, lakini mapato halisi ni kama hayo tuliyomwambia, mchango wa asilimia 20 SMZ ambao wamepata milioni 432,802,044. SMT imepata mgawanyo wa asilimia 30 ambayo ni milioni 649, 203,660, lakini Mamlaka yenyewe inapata asilimia 50 ambayo inakuwa ni bilioni 1,082,006,100.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, hili la mapato ya Uvuvi wa Bahari Kuu, hata tukiendelea kujadiliana hapa hatuwezi kupata ufumbuzi. Kwa hivyo, nadhani niiombe kamati yetu na Mhe. Mwenyekiti ananitizama vizuri pale Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Kudumu inayohusika na sekta hizi au wizara hii, ilifanyie kazi kwa kina na baadaye ije itushauri hapa Barazani kama kweli kuna uhalisia wa mapato haya.

Vile vile kama nilivyosema kwamba watizame na ripoti za mapato zinazoripotiwa baina ya hapa na Bunge na Mawaziri wanaohusika na kwamba je, tuna sababu ya kuendelea nalo hili kuiendesha kiutalawa kwa pamoja na wenzetu, kwa sababu kama tunavyojua kwamba suala la uvuvi si la muungano kwa sababu ile ni biashara.

Lakini narudi katika lile la mwanzo kuhusu mapato. Mhe. Mwenyekiti, mimi maelezo ya Mhe. Waziri namshukuru, kwamba kiasi fulani amenipa mwangaza. Sasa majibu yake anapozungumza kwamba kuna mapato ya

kurugenzi yaingie katika Wizara mimi nashangaa Mhe. Mwenyekiti, kwamba hivyo kuna mapato ambayo yanajua kurugenzi tu na wizara haijui na huu ndio utaratibu gani wa kiserikali?

Mhe. Mwenyekiti, haya ambayo tumepitisha hapa na tumesomewa fungu la kwanza, pili, tatu na mpaka hapa nilipopiga buti mimi yote haya ni mapato ya kurugenzi au idara, ambayo kwa jumla yake ndio yanafanya mapato ya wizara. Sasa tusirefushe mjadala, isipokuwa naomba anihakikishie jambo moja kwamba je, wakaguzi, yaani Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Wizara na Mkaguzi wa *CAG* wanaruhusiwa kuzifanyia ukaguzi fedha hizi katika hiyo kurugenzi.

Pili nimuombe Mhe. Mwanasheria Mkuu akae nao na waliharakishe haraka sana hili, kama kuna Kanuni au Sheria yoyote kama ni kweli na mimi siamini kama kuna sheria inatoa mwanya kurugenzi kukusanya mapato na baadaye ikajua yenyewe tu na ikatumia yenyewe na Mkurugenzi wake na sisi ambao tunasimamia mapato na matumizi ya wananchi ya Zanzibar tukiwa hatujui, basi huo ni wizi wa fedha za umma za wananchi wa Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama kuna sheria hiyo sifahamu na wala sijui kama kuna sheria inatoa mwanya wa kulikiuka Baraza hili katika fedha ambazo zinazohusu wananchi wa Zanzibar. Sasa kama kuna mwanya huo au kwenye kanuni basi uharakishwe, ili fedha zote ziripotiwe katika wizara na baadaye zije zithibitishwe na Wawakilishi wa wananchi, na Mhe. Mwenyekiti hakuna mtu ambaye yuko juu ya sheria anayeruhusiwa kuweka mkono wake katika mapato ya wananchi hii bila ya Baraza hili kujua hakuna utaratibu huo.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nasema tuendelee ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na nimesikia maelezo ya Mhe. Mjumbe, kwa ufupi ni kwamba tulikaa na Mkaguzi wa Wizara na tukaligundua hilo kwamba hakuna ile *transparency* na tulisema hapana lazima tuibadilishe hii Kanuni, ili tuone kwamba hii *transparency* inaonekana moja kwa moja na wizara, kwa ajili ya kudhibiti hiyo hali kwa sababu niliwaambia kwamba atakayejibu ni Waziri. Kwa hivyo, lazima mambo haya na wizara ifahamu na kanuni hii lakini bado haijatoka.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe awe na subra na nadhani tutakuja kuiona hiyo Kanuni kwamba ni kiasi gani itadhibiti hayo mapato kwa maeneo hayo ya hifadhi. Kwa hiyo, Mhe. Mjumbe nafikiri uridhike na hilo na tufanye subra na tutalitekeleza, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, tunakushuruku. Tuendelee.

Kifungu 0016	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja	430,000,000/=
Kifungu 0601	Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja	59,000,000/=
Kifungu 0701	Idara ya Mazao ya Baharini Unguja	70,000,000/=
Kifungu 0801	Idara ya Uzalishaji Wanyama Unguja	9,000,000/=
Kifungu 0802	Idara ya Uzalishaji Wanyama Pemba	6,000,000/=
Jumla ya Fungu		**613,000,000/=**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0010 Idara ya Mipango Sera na Utafiti

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana jana nilipokuwa nikichangia kwenye sehemu hii nilizungumzia kwamba aliyekuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Said Ali Mbarouk alitembelea katika ziara zake na mimi nilishiriki kwenye ziara hiyo katika Kisiwa cha Kojani. Kwa kweli kwenye majumuisho yetu basi mwenyewe alivutiwa na akatoa ahadi kwa wananchi wale kwamba apatiwe watu wawili kwa ajili ya kwenda kusoma Chuo cha Uvuvi na hilo lilifanyika.

Lakini kwa bahati mbaya na masikitiko makubwa kuwa Wizara inasema mipango hiyo haijui wakati tulikuwa na Waziri mwenyewe na alifuatana na maafisa wake na Mhe. Farida Amour Mohammed ni shahidi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka wizara iniambie vijana hawa wawili waliopendekezwa na Mhe. Waziri ni lini watapata nafasi hiyo ya kwenda kusoma na kulipiwa na akinieleza suala hilo basi sina matatizo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na nimesikia *concern* ya Mhe. Mjumbe na mimi niseme tu kwamba nafikiri angewaleta hao vijana wawili na halafu tuangalie bajeti yetu na tuone vipi tunaweza kuwasaidia, na nia ya kuwasaidia ipo pale pale, labda itakuwa yamekosekana mawasiliano, lakini hatuna nia ya kumkomoa mtu.

Kwa hivyo, ni vyema Mhe. Mjumbe tukashirikiana baada ya bajeti hii, basi tuje tuzungumze na awalete hao vijana na tushirikiane na tutizame nini wizara itafanya kwa kuwasaidia vijana hao. Mhe. Mwenyekiti, nashukuru.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, mimi sina wasi wasi na tamko la Mhe. Waziri, isipokuwa nataka anithibitishie ndani ya Baraza hili la Wawakilishi, kwamba ni lini baada ya kumaliza kikao hichi mimi na yeye

tukutane, ili vijana hao wapate nafasi kwa sababu iliyosema pale ni serikali kupitia wizara.

Kwa hivyo, ninaamini serikali haiwezi kuwadanganya wananchi wake. Sasa atoe tamko rasmi kwamba ni lini tukutane mimi na yeye kwa ahadi na mimi niko tayari kutokwenda Pemba, lakini jambo hili limalizike. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, *inshaallah* mara tu tutakapomaliza bajeti basi Mhe. Mjumbe anitafute. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipopeleka mchango wangu wa maandishi nilimuomba Mhe. Waziri anieleze kwa nini Wakuu wa Idara hawapati posho? Wakati kazi zao ni ngumu na wameaminiwa kupewa kazi ya kuiongoza idara. Lakini kwenye majumuisho ya Mhe. Waziri sikupata jawabu, kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti naomba Mhe. Waziri anipe majibu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru ni kweli labda kuna baadhi ya hoja sikuwahi kuzisoma, lakini vyovyote vile nafikiri baada ya bajeti tukae na tuzungumzie kuhusu hilo suala, kwa sababu sijaliona hapa na nimejaribu kutafuta. Lakini kubwa ni kwamba tutahakikisha au tutajaribu kutizama ni kiasi gani tutaweza kuwasaidia kwa maposho yao. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe anipe subira kidogo. *(Makofi)*

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, hapa ndipo panapotakiwa kutolewa majibu kwa sababu tunayo kazi ya kupitisha mafungu na mimi nimo katika kuwatetea wananchi kupata haki yao. *(Makofi)*

Kwa hivyo, siwezi kusubiri nikapata majibu baadaye, kwa maana hiyo namuomba Mhe. Waziri anijibu na serikali yote ipo kwa sababu wakuu wa idara ndio watu wanaosaidia uongozi wa wizara kufanya kazi. Vile vile kuna tarishi ambaye analipwa posho, karani wa masjala ya siri analipwa posho, dereva Afisa Mdhamini analipwa posho, lakini Wakuu wa Idara ambao ni wenye dhamana kubwa hawalipwi posho. Kutokana na hali hiyo, naomba nisaidiwe hapa, ili niweze kupitisha fungu. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa maelezo yake. Aidha nimshukuru Mhe. Salma Mohammed Ali kwa namna alivyo mahiri anavyowatetea wafanyakazi wa serikali, nataka nimpongeze sana. *(Makofi)*

Vile vile nataka nimhakikishie kwamba ni nia ya serikali kuona kwamba wafanyakazi wake wote wanapata haki zao wakiwemo wakuu hawa wa vitengo na idara mbali mbali.

Kwa hivyo, nimuombe tu Mhe. Salma Mohammed Ali, kwamba atupe muda tulifuatilie jambo hili kwa undani wake tuone kasoro zilizojitokeza na kwa nini walikosa kupata haki zao, ili marekebisho yafanyike na hazi zao wazipate kwa mujibu wa sheria zilizopo na kwa mujibu wa taratibu za sasa zinazochukuliwa kuhakikisha kwamba wafanyakazi wanapata maslahi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Mjumbe atupe muda kwa ajili ya kulifuatilia jambo hili, na ninamuhakikishia kwamba serikali itachukua kila hatua kuwa mwenye haki yake basi apate haki yake.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nimemfahamu sana Mhe. Waziri na kwa vile amesema kwamba suala hili watalishughulikia basi sina tabu. Lakini namuomba Mhe. Waziri aniambie kwamba litafanywa lini na vipi zile haki zao za nyuma watazipata? Naomba maelezo zaidi na baada ya hapo tuendelee. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba zoezi hili litaanza mara, yaani kuanzia leo tutawasiliana na wizara husika inayosimamia masuala ya Utumishi wa Umma na wakati huo huo, ili waweze kuwasiliana na wizara husika kwa ajili ya kuona na kujua kasoro na tatizo liko wapi.

Kwa kweli nataka nimhakikishie kwamba haki zao zote na zikiwemo za nyuma kama walikosa basi itabidi wapewe, kwa kufuata sheria zilizopo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana jana wakati nilipokuwa nikichangia kwa masikitiko makubwa nilisema kwamba unapoboresha uvuvi katika nchi imefanya *three in one*, yaani umemuwezesha Mvuvi, Mchuuzi na Mama lishe, kwa sababu pale kwenye madiko wanakuwepo na kufanya shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka nimuulize Mhe. Waziri katika hii, sisi inaonekana hatuko makini katika kuuboresha uvuvi na kuwasaidia wananchi. Hivi iweje wale Wasukuma kule waweze kufanya zile *Fish Fillet Industry* tena samaki wao wanategemea wale Sato na Sangara kuna ndege zinakuja kutoka nje na kuja kuchukua *Fish Fillet*.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nenda kwenye hoja moja kwa moja muulize Mhe. Waziri.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni hoja, na niko katika kujenga hoja. Hivi ni kwa nini wenzetu Wasukuma waweze kujenga Viwanda vya Kusindika Minofu ya Samaki kule, ambapo wao wana aina mbili tu za samaki Sato na Sangara na sisi huku tushindwe ni kwa sababu gani ni umasikini wa serikali yetu au wawekezaji hawataki kuweka *Fish Fillet* kwa samaki ambao wako baharini?

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, *concern* ya Mhe. Mjumbe tumeisikia na labda alikuwa hayupo na alijibiwa vizuri sana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kuwa sasa ujumbe mmoja upo hapa, na hivi sasa serikali inatafuta wafadhili juu ya kujenga Kiwanda cha Samaki. Vile vile kama alivyoona kwamba Bandari ya Samaki tayari na tumetiliana mikataba na *JICA* na hizo ndizo hatua ambazo tunazokwenda nazo na wala hatuwezi kufika hatua 1000 kabla ya kuanza hatua moja. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, hii *echo* inafanya nisisikie vizuri na wala sikulisikia jibu. Lakini kwa sababu nimesikia kidogo tu kwamba kuna mpango. Kwa hivyo, mimi napenda kusema kwamba *Fish Fillet* zinaingiza fedha na ukishatoa ile minofu, basi vile vichwa vinatumika kwa ajili ya kutengeneza chakula cha mifugo. Sasa nyinyi musituweke masikini na tukalala na njaa wakati kitu tunacho. *(Makofi)*

Sasa yale mapezi …

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri na kabla ya hapo Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kwamba upo mpango wa kuwa na Kiwanda cha Samaki hapa Zanzibar na wataalamu tayari wapo, turidhike na hilo na tuendelee mbele na halafu mengine tutafanya baadaye. Lakini tayari mpango upo kwa mujibu wa swali lako ulivyouliza na vile alivyojibu Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, unajua hii *gelotive* si nzuri na ilikuwa ni ufahamu na wewe Mhe. Mwenyekiti unipe maelezo niridhike, ili turuhusu, sasa kama wewe Mhe. Mwenyekiti, umeamua apite tu sawa. Lakini mimi nataka kujua hizo *Fish Fillet Industry is ok. So what about Canning Industry*? (*Makofi*)

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, tayari tumeshazungumza vya kutosha sana, kwa sababu ni utaratibu mzuri ambao

tunaokwenda na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko amezungumza. Vile vile tumesema baada ya kiwanda hicho kuja hapa basi wataalamu watatushauri na mambo mengine ya kuweza kufanya.

Kwa hivyo, hivi sasa tuna mpango mkubwa na tayari tumeshatia saini kuweza kupata Bandari ya Uvuvi peke yake na viwanda ambapo wataalamu wapo. Lakini wakiwa wanakuja wawekezaji watatushauri tufanye nini kwamba mapanki yatakwenda wapi na minofu itakwenda wapi, watatushauri kama mapanki yatakuwa wananchi yatawafaidisha basi minofu itachukuliwa basi wao watatushauri kwa sababu wao ndio wawekezaji na sisi hatuna viwanda.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Tunaendelea.

Kifungu 0010	Idara ya Mipango Sera na Utafiti Pemba	51,200,000/=
Kifungu 0011	Idara ya Uendeshaji na Utumishi Pemba	600,500,000/=
Kifungu 0012	Idara ya Mazao ya Baharini Pemba	

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipochangia nilizungumza kuhusu wafugaji wa samaki (mabwawa ya samaki) na Mhe. Waziri amejitahidi sana kujibu. Lakini nilivyokusudia mimi nilimwambia kwamba lengo na madhumuni wafugaji wetu si kufuga kitoweo tu, isipokuwa ni kufuga kwa ajili ya biashara ambayo itaingiza faida kwa serikali pamoja na wananchi.

Sasa wananchi wanajitahidi kutengeneza mabwawa na yapo mabwawa ya kutosha kwa ajili ya kufugia samaki. Jambo la kusikitisha ni kwamba wale samaki wa kufuga hawana isipokuwa wanafuga samaki ambapo wanaingia samaki wa kila aina kama vile mizira, kaa, mizira wanakula samaki wale wadogo wadogo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anieleze kwamba watafanya vipi kuhakikisha kwamba wanayo mabwawa. Kwa mfano, Unguja kuna bwawa moja na Pemba kuna bwawa moja la kufugia samaki, ili wapate wale samaki wadogo wadogo (vifaranga) na kuwapa watu kwa ajili ya kufuga samaki ambao ni wa uhakika na sio wale samaki wanaoingia na wanakula wenzao, isipokuwa kuwe na samaki ambao ni maalum, ili serikali ipate faida na wananchi waweze kujiwezesha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kwamba anihakikishie kuwa yeye atajenga bwawa moja la mfano la kufugia samaki wadogo wadogo (vifaranga) Pemba na Unguja, ili wananchi wasipate tabu na wapate samaki maalum wa kufuga na sio samaki tu ambao wanafugwa na halafu wanakula wenzao. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na tumemsikia Mhe. Mjumbe, ni kweli suala analolizungumza. Kwa kweli moja ya mtihani au changamoto ya Sekta hii ya Ufugaji Samaki ni namna ya kupata samaki wadogo (vifaranga), kwa sababu vifaranga kwanza ni kitu *delicate* kukihamisha kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyengine kuna mitihani yake mara vinakufa, pengine umechukua ukapata pengine 10 kitu kama hicho.

Hata hivyo, wizara au serikali kwa jumla tayari tumeshatiliana saini na kampuni moja ya Kichina ambayo ujumbe wake unakuja karibuni hivi. Miongoni mwa mambo moja ni kutengeneza *incubator*, yaani *Center* za Kuzalisha Samaki Wadogo Wadogo (Vifaranga), ambayo ni ya uhakika kabisa.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe aelewe hilo na aone kwamba wizara tumeliona na ndio maana tukauagiza mradi huo uwepo, kwa ajili ya kupata usalama wa samaki wadogo wadogo (vifaranga) kwa wafugaji wetu na wawe wanafanya ufugaji kwa uhakika na wajue wapi wanakwenda kutafuta samaki wadogo wadogo (vifaranga).

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa ni kazi ya kubahatisha tu, sijui bwawa fulani wapo, yaani ni kuokotaokota tu bado hakujawa na uhakika hasa, na wale wengine waliofanikiwa kwa kweli ni juhudi zao na ninawasifu sana.

Sasa ili kuwarahisishia tayari mradi tumeshatiliana saini na kampuni moja ya Kichina ambayo itakuja hapa nafikiri mwezi wa Agosti wataingia hapa, kwa ajili ya kwenda kufanya *feasibility study* Pemba na kuwa na *Farming Fish Centers* kwa ajili ya uzalishaji wa samaki wadogo wadogo (vifaranga). Hali hiyo yote ni kwa sababu tunawajali watu wetu na tunataka kuona sekta hii ya ufugaji wa samaki inakua siku hadi siku. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, leo ni siku ya Ijumaa na rafiki yangu sitaki nimsumbue sana. Lakini nataka kauli yake anayoisema iwe ni kauli sahihi na isiwe kwenye kitabu, iwe ni kauli ambayo inatekelezwa na inatekelezeka. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Tuendelee.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi wakati nilipokuwa nikichangia Soko la Tumbe nilielezea mapungufu na athari zake na ninamshukuru Mhe. Waziri amejaribu kunipa majibu mazuri tu pamoja na Mhe. Naibu Waziri kwamba tayari wameshafungiana mkataba na mkandarasi kwamba hadi Agosti 13 kuwa soko lile liwe tayari limeshafanyiwa marekebisho, vyenginevyo kama halikufanyiwa marekebisho basi watatoa *penalty*.

Mhe. Mwenyekiti, nimeridhika na majibu, lakini pamoja na hayo tunakuwa tunapata mashaka na wasi wasi mwingi sana kwa Mawaziri wetu, yaani majibu yanakuwa mazuri na vitendo vinakuwa havina muelekeo. Mhe. Mwenyekiti, nazungumza hivyo kwa ushahidi, tumeshazungumza sana hapa suala la *airport* na kila siku tunaambiwa kwamba watafiti wameshakuja na mpaka leo bado. *(Makofi)*

Vile vile kuna soko jengine huko Wete Pemba, ambalo tayari limeshajengwa na limemalizika na mpaka ufunguaji halielewi. Mhe. Mwenyekiti, huko Pemba kuna jengo la Wizara ya Fedha limeinama na mpaka leo halieleweki. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, labda Mhe. Waziri anieleze kwamba kikao kijacho tukijaaliwa uhai ukiwepo kama ile hatua ya wizara itakayochukuliwa basi atatuletea taarifa, ili Wajumbe tujiridhishe na kuondoa zile dhana za wasi wasi kwa wizara nyengine. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala hili tayari liko kwenye *pipeline* na mimi naahidi kwenye kikao kijacho, basi tayari itakuwa tumeshalimaliza kwa sababu wale watu tayari tumeshatiliana mikataba na kuna fedha zao ambazo tumezizuia na tutaanza kama ilivyopangwa na wala tusiwe na wasi wasi, kwamba tutalitekeleza hili na kipindi kijacho cha Baraza tutakuta tayari tumefikia hatua nzuri. *(Makofi)*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. Tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia eneo hili nimeridhishwa kidogo na suala la Soko la Tumbe. Lakini kuna jambo muhimu mno ndani ya soko hili, yaani ni mtambo wa baridi.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, anieleze Mhe. Waziri kwamba ni lini mtambo huo utapelekwa Pemba na

mimi nikiwa Mwakilishi wa Jimbo lile la Wete atanishirikisha kuwa shuhuda wa jambo hilo. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, mtambo huu upo wizarani tumeuhifadhi na mara tu baada ya kukamilisha marekebisho ya jengo, basi nitamshirikisha Mhe. Mjumbe, ili twende tukakabidhi pamoja kule, yaani mradi wa Tumbe pamoja na Mhe. Mwakilishi wa Tumbe pia kwa sababu yeye ndiye muhusika zaidi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, tunakuombeni muwe na subra na tusubiri marekebisho ya jengo yafanyike na halafu tutashirikiana katika kuuweka mtambo tena upo.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa mtambo huu ni wa Soko la Tumbe na Wete kuna ofisi ya wizara hii nzuri kubwa yenye eneo zuri la kuhifadhi, ridhaa yangu nilitaka Mhe. Waziri aniambie kwamba mtambo utahifadhiwa kwenye ofisi ya wizara hii iliopo Wete Weni, wakati tukisubiri matengenezo ya hilo soko ambalo halijulikani lini litamalizika, ningependa nipate jibu la namna hiyo.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mhe. Mjumbe anataka kuridhika, ili aone kwamba unakwenda kuwekwa Wizara ya Mifugo na Uvuvi Weni Pemba. Kwa hivyo, tutaangalia hali ya *store* pale kama inaridhisha basi tutauweka kabisa huko na tutashirikiana mimi na yeye kama *store* inaridhisha basi tutauweka.

Mhe. Asaa Othman Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nina imani kubwa na Mhe. Waziri na Naibu wake na bila ya kupoteza muda wako, nataka tuendelee isipokuwa baada ya hafla hii Mhe. Waziri atamke kwamba ataonana na mimi kwa ajili ya kuweka mazingira safi. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, *inshaallah* tutaonana.

Kifungu 0012	Idara ya Mazao ya Baharini Pemba	76,500,000/=
Kifungu 0013	Idara ya Uzalishaji Wanyama Pemba	

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, jana wakati nilipokuwa nikichangia nili-*declare my interest* kwamba mimi ni miongoni mwa wafugaji. Sasa katika kuboresha mazao ya mifugo hulazimika kutumia mbegu za nje kupitia *artificial insemination*. Vile vile tunao madume chotara ambao takriban hivi sasa wana karibu asilimia 75 ya zile *exotic genes* ambao huwa tunawatumia kwa kupandishia mifugo yetu.

Kutokana na kwamba hawa madume tunawapa shida kwa sababu anaweza aka-*serve* si zaidi ya ng'ombe 15 kwa siku na tunamu-*over work*. Je, ni lini wizara hii Mhe. Mwenyekiti itatufundisha sisi wafugaji wa kienyeji huko vijijini, kwa mfano kule kwangu Vitongoji kuweza kuvuna zile mbegu za uzazi kutoka kwa yale madume chotara na kukaweza ku-*inseminate* wenyewe, kwa sababu *one ejaculation* inaweza ku-*serve* hata ng'ombe 10. Lakini tukimuachia akiweka yeye mwenyewe zile mbegu kwa yale majike inabidi anatumia mara moja tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sasa ni lini watatufundisha sisi wakulima au wafugaji kuzivuna zile mbegu na kuweza kuzitia kwa ng'ombe wetu na kwamba mvuno mmoja tunaweza tuka-*serve* kwa ng'ombe wengi? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti,

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo la kitaalamu kwa kumfundisha kila mmoja inakuwa ni ngumu kwa sababu pale tunatumia *preservatives agency* ambayo ndiyo *liquid nitrogen*. Kwa hivyo tunataka dume lenye asilimia mia la kuzalika zile mbegu zenyewe. Kwa sababu mbegu zenyewe kuna *motility* ambayo zile *spermes* zinakwenda vizuri na kuna wengine kama *Azoospermia, Oligospermia, Necrospermia.* Hivi vitu sio vya kawaida. Sasa kwa kuweza kumfundisha kila mmoja inakuwa ni vigumu. Lakini kama anao watu wawili watatu wa lile eneo lake basi mimi namuahidi kuwaleta tukawafundisha wale wanaohitaji tutakuwa nao, tutawafundisha halafu wataweza ku- *serve* vizuri.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mimi ni mshamba wa kule Vitongoji nafikiri huwa sifahamiki vizuri humu ndani. Nililokusudia sio kila mmoja ni sisi wafugaji, sio kila mmoja kwamba ni mfugaji katika nchi hii. Lakini kwa sababu kasema apelekewe basi *Inshaallah* tutampelekea na katika hili basi tuendelee.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nina masikitiko rafiki yangu nilimuuliza swali langu, lakini hata kule kulijibu hakulijibu.

Nilimuuliza Mheshimiwa katika kuwaendeleza wafugaji kama mtu anapewa mbuzi mmoja au kuku mmoja, hivi tunakusudia kuwa tunawaendeleza au tunawapa watu wale nyama tu. Nikamuuliza kutokana na kuwa mtu amepewa kuku mmoja au mbuzi moja, na hatuoni faida inayopatikana, nilitaka Mhe. Waziri anijibu kwamba ni kiasi gani cha fedha kinachotumika kwa kununua mbuzi mmoja mmoja na kuku. Pia nikataka anambie ni faida gani tunayoipata

kutokana na hao watu wanaopewa mmoja mmoja. Lakini bahati mbaya sijui kama kalisahau au ni kwa bahati mbaya ipi lakini sikupata jibu lolote lile.

Lakini kulingana na hali ilivyo ya Ijumaa basi namuomba tuendelee nilikuwa namkumbusha tu niweke sawa *hansard*.

Kifungu 0013	Idara ya Uzalishaji Wanyama Pemba	73,000,000
Kifungu 0014	Idara za Huduma za Utibabu wa Mifugo Pemba	70,000,000
Kifungu 0015	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Pemba	82,500,000
Kifungu 0016		

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kabla ya kujenga hoja yangu kwanza nilikuwa naomba uniruhusu nizungumze machache Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kwanza. Kuna jambo muhimu ambapo linahusu wananchi wetu katika hospitali ya Mnazi Mmoja kuna taarifa tumeipokea hivi sasa, leo ya tatu *Operation* Kuu Mnazi Mmoja haifanyiki kutokana na sababu ya *Oxygen*. Nilikuwa nikisema siku zote hapa Mawaziri, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu watembelee vitengo vyao. Hili ni jambo la kusikitisha.

Mhe. Mwenyekiti, hili swali limekuhusu wewe kama ni Mwenyekiti, wa Wizara hii ya Wanawake na Watoto na Ustawi wa Jami, leo ya tatu kuna *operation* zimesimama tena *major operations*. Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nijenge hoja yangu.

Huu ni mwaka wa tatu tokea kuingia kwenye Baraza hili, nilikuwa nikihoji boti ya wananchi wa Jimbo la Muyuni au wananchi wa Muyuni, boti yao ilikuwa haipo imepelekwa Kizimkazi na nikaambiwa na Mhe. Naibu Waziri kwamba alifanya jitihada kubwa akatupatanisha na wananchi wangu na suala hili likaonekana kama limemshinda, na kakiri hivyo na akaniahidi kuwa atanipatia boti. Wale wananchi mimi nimeshawaahidi kuwa boti itapatikana. Anambie tu sitaki kuja kusimama tena kwa mara ya pili na leo ni Ijumaa. Anambie ni lini wananchi watapata boti hiyo? Ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli Mhe. Jaku alitoa hoja hiyo mwaka jana. Lakini vile vile nilimkutanisha au tulikutana na wale wavuvi wenyewe, ile boti walipewa lakini kutokana na makundi ambayo yalikuwepo pale mimi nilikutana katika ukumbi wa juu wa Kamati yeye pamoja na watu wake wote kumthibitishia kwa maofisa wangu kwamba ile boti wamekabidhiwa.

Sasa nimwambie kwamba kuna harufu ya mradi fulani imetokea, sasa kama utatokea hiyo sisi tuko tayari kumsaidia ili kuondosha ule mzozo mzito wa pale kwenye Jimbo lake ili tuweze kuwapa boti ile. Lakini sasa hivi hatuna mradi tuna harufu tu, lakini ukitokea sisi tunaahidi kumsaidia wakati wowote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Waziri, mimi ninamuamini wala sina mashaka naye na leo ni siku ya Ijumaa. Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, jana nilipokuwa nikichangia nilizungumzia sheria ya Nam.7 ya mwaka 2010 kwamba sheria hii imekuwa ni kikwazo kwa wavuvi wetu, haitekelezeki, kutokana na mikakati iliyokuwemo ndani ya sheria.

Vile vile nikazungumzia kuwa tarehe 3/07/2012 Jumuiya ya Maendeleo ya Wavuvi wa Kojani walifanya Mkutano katika Ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Kongwe na Mhe. Makamo wa Pili wa Rais alialikwa. Lakini kwa bahati mbaya kutokana na majukumu aliyokuwa nayo hakuweza kufika alimuakilisha Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na akasema yote ninayoyapata nitampelekea Mheshimiwa. Lakini jambo la kusikisha na la hudhuni kabisa ni kuwa hakuna ripoti yoyote. Mheshimiwa alikuwa na kiredio chake kidogo akasema narikodi hii nitakwenda kumpelekea.

Wavuvi wa Mikoa mitatu wa Mjini Magharibi walikutana hapo kilio chao ni hicho. Je, Mhe. Waziri ni lini kwa sababu sheria hii ina mapungufu makubwa italetwa hapa Barazani ili kufanyiwa marekebisho. Naomba jawabu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, nafikiri Mhe. Mjumbe alikuwa hayupo *hadhir* nilipokuwa natoa maelezo, kwamba tayari tumeshatengeneza kanuni na hii kanuni ime- *accommodate* mambo mengi, pamoja na hayo ambayo labda anahisi kwamba yanamkereketa. Kwa hivyo Mhe. Mjumbe ungesubiri tu ukaiona hii Kanuni baada ya kutoka kwa Mwanasheria Mkuu akishasaini uone kiasi gani imejaribu ku-*stream line* yale makali, halafu kama kuna neno zaidi hadi utapokuja kuzungumza. Lakini tayari kanuni ipo kwa Mwanasheria Mkuu na itakapokuja ndipo utakapoona kiasi gani imekidhi zile hoja zako. Kwa hivyo nakuomba Mhe. Mjumbe uwe na subra ili tuone kanuni hiyo inasemaje. Ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru tena. Kauli ya Mhe. Waziri ni nzuri lakini jana nilitoa mfano ulio hai. Nilisema mtu umemuweka ofisini, anafanya kazi ukamzuilia kalamu, ukamzuilia kompyuta, huyu atakuwa anafanya kazi? Leo wavuvi wanavua ukamzuilia chupa kwa ajili ya kupata hewa, unamzuilia viatu vya kuogelea, je, huyu unataka afanye kazi au unataka kumuua?

Lakini vile vile wanazuiliwa kioo lakini kwa wazungu inakuwa ni halali. Kwa sababu mzungu anapokwenda kwenye *Coral* ni lazima avae kioo. Sasa hebu tuthibitishie hiki kioo kinaharibu mazingira namna gani na kioo kile kinakufanya uone vizuri ndani ya bahari, bila ya kioo huwezi kuona, sote ni wavuvi na kila aliyepitia uvuvi analijua hilo.

Nataka Mhe. Waziri atwambie hasa, hapo ndio nitashirikiana naye kwa ukaribu kabisa, lakini atwambie ni lini mambo haya yatafanyika na kuweza kufanya kazi kama kawaida ili wavuvi wetu waendelee vizuri. Kwa sasabu kina tunapokwenda kwenye uvuvi wa bahari kuu lakini nimesema ni mpango wa muda mrefu. Na wavuvi wetu ni waluga luga hawafikii huko nataka wakifikia huko hakuna matatizo. Mheshimiwa naomba jawabu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tumepiga marufuku juu ya vifaa hivyo ambavyo amevizungumza. Ukweli ni kwamba sio kwamba vile vifaa ni haramu, vifaa si haramu, haramu ni yale matumizi yake. Ataona labda watalii wanakuwa navyo viatu, vioo, kwa sababu wao hawavitumii kwa njia hiyo, wao hawatumilii kwa kuvulia wao wanavitumia zaidi kwa kuangalia *coral*, kuangalia matumbawe, kuangalia *dolphins*.

Kwa sababu kioo siku zote kinadanganya, samaki hata akiwa mdogo gani unapomuangalia kwenye kioo basi anakuwa mkubwa. Kwa hivyo anakuhadaa wewe unaona bora nimpige huyu.

Tumekataza bunduki kwa sababu bunduki kwa vyovyote samaki ana *nature* ya kwamba hatulii, maisha samaki hatulii. Kwa hivyo mvuvi wa bunduki samaki anayempiga ni yule ambaye katulia, na ukimuona samaki katulia basi juwa ni mjamzito. Kama mjamzito maana yake mle ndani ya tumbo kabeba mayai si chini ya elfu. Unapompiga umefaidika kupata samaki yule lakini angalia umeua viumbe vingapi, mayai yale je, angeyatotoa tungepata samaki wangapi.

Kwa hivyo naomba Mhe. Mjumbe aridhike na hili lakini hata hivyo tusubiri kanuni, utaona imekidhi kiasi gani.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze, mimi katika fani ya uvuvi naijua. Sehemu nnayokaa Kikwajuni nimekaa zaidi ya miaka mitano kwa uvuvi, na hakuna mwamba hata mmoja Unguja nisioujua. Sasa nataka Mhe. Waziri yeye na Naibu Waziri na watendaji wake tuingie katika mambo ya utafiti, tujue kioo kinatumika vipi ndani ya bahari na mimi nikiwemo ndani ya boti, mimi nivae kioo na yeye avae kioo, tuangalie kioo

kinatumika kwa matumizi gani. Akinithibitishia hapo niko tayari. *(Vicheko)(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hiyo Mhe. Hassan tuendelee, hujasema tuendelee au unataka majibu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Anipe majibu hajanambia kama ataingia botini. *(Vicheko)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, ukubali tu kwamba utakwenda naye.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Tuko tayari, Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan, umeridhika na jibu la Mhe. Waziri.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Nimeridhika anambie ni siku gani, ili tuingie mimi nikatayarishe boti akaangalie viatu vinatumika vipi na kioo kinatumika vipi.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Tusubiri tumalize bajeti.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda wetu uliobakia ni mdogo naomba nimuombe Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aweze kutengua kanuni ili tuweze kuendelea. Vile vile kuturuhusu katika hicho kipindi cha nusu saa ambayo tunaiomba kuweza kumaliza mafungu kwa jumla.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe kwa kuwa muda ulio mbele yetu hautoshi kumalizia bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Na kwa kuwa leo Ijumaa, kwa hiyo niombe Baraza lako tukufu tuweke kanuni ya muda kando ili tuweze kutumia nusu saa, ili tuwahi kupitisha mafungu na tuwahi kwenda Msikitini Kusali.

Waheshimiwa naomba Waheshimiwa Wajumbe wakulibaliane kwamba kuanzia sasa tuongeze nusu saa maana yake mpaka saa sita na robo (6:15) iwe tumemaliza bajeti hii tuweze kuwahi msikitini. Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naafiki.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia katika sehemu hii ya Idara ya Maendeleo ya Uvuvi, nilizungumzia suala la ufisadi katika usajili wa meli za uvuvi. Kwanza naomba nikuhakikishie kwamba sitochukua muda mrefu katika hoja hii. Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi pamoja na Naibu wake kwa maelezo ya kina na kwa uwazi kabisa kulieleza suala hili katika Baraza hili na kwa wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwanza kutokana na majibu aliyokuwa ametupa na taarifa ambazo nilizisema jana kwamba nimezipata katika mtandao. Naomba mimi binafsi na niwaombe Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi tuungane kwanza kumpongeza sana kijana wetu huyu Zahor Mohamed El-kharousy kwa kazi kubwa aliyoifanya. Si rahisi Mhe. Mwenyekiti, katika vishawishi vingi vilivyokuwepo katika mambo haya mtu ukaweza kusimamia haki na uadilifu. Kwa vile leo ni siku ya mwezi 17 Ramadhani, siku ya Ijumaa na leo ni siku ya vita vya Badri, basi kuwapongeza wanaosimamia haki inafaa sana siku ya leo.

Mhe. Mwenyekiti, katika majibu yake Mhe. Waziri na Naibu Waziri wametwambia kwamba suala hili baada ya kuripotiwa kwanza katika Tume hii ya *Indian Ocean Tuna Commission (IOTC)* na baadaye kuripotiwa katika jeshi la polisi kuchukua hatua, sasa suala hili lipo katika uchunguzi wa polisi.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nihakikishiwe mambo mawili ili tuendelee. Kwanza katika majibu na katika vielelezo ambavyo kanisaidia Mhe. Waziri na Naibu wake, nimeona hii *complain* imefunguliwa kwa jina la mtu binafsi la Zahor Muhammed Kassim. Mimi nilikuwa nadhani kama ingelikuwa sahihi kwamba taasisi kama ina mamlaka ndio inafungua *complain*. Haidhuru kwamba itakuwa na mtu ambaye anatoa taarifa. Kwa sababu kuna hatari ya watu wenye nia mbaya, ikaonekana kwamba ni suala binafsi na ndio hivyo alivyotwambia kwamba kukawa na vitisho. Kwa hivyo nilikuwa nadhani hilo lingewekwa vizuri.

Lakini hapo hapo nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye mwenye dhamana ya Taasisi za Muungano, hili alifuatilie kwa karibu. Kwa sababu tunaposema uchunguzi unaendelea na wanaohusika na mambo haya ni watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha. Tunajua taasisi zetu mara nyengine zinavyoathiriwa na masuala ya rushwa. Linaweza hili likafifia hivi hivi Mhe. Mwenyekiti. Kama uchunguzi ukitizama kwenye nyaraka ambazo zimo kwenye Tume tayari zinaonesha vielelezo vyote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba mambo mawili; moja kwamba tuhakikishiwe kwamba suala hili litafuatiliwa kwa kina sio tu na Mamlaka lakini Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ambaye ndiye mwenye kusimamia jeshi la polisi kwa upande wa Zanzibar katika taasisi za Muungano, ahakikishe kwamba suala hili tunalijua limefikia wapi mwisho wake. Na kwa sababu uchunguzi umeshafanyika na vielelezo vipo vinaonekana vya kitaalamu kabisa isije ikawa funika funika.

Lakini la pili niombe serikali impatie ulinzi kijana huyu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu ndugu Zahor Mohamed El-Kharousy kwa kufanya kazi kama hii, watu kama hawa ambao mara nyengine wanajiingiza katika mambo makubwa makubwa inaweza ikawa ni *mummify* Mhe. Mwenyekiti, waweze kumlinda ili usalama wake ubakie na uhakikishwe kwa kadri inavyowezekana katika mikono yetu sisi binaadamu. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Ismail Jussa Ladhu, kwa namna anavyofuatilia mambo mbali mbali hususan yanayohusu maslahi ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba ushauri wake tunaupokea, tutaufanyia kazi na tutawasiliana na Mwanasheria Mkuu hapa, ili tuone hili suala la kwanza kwamba tunaweza kubadilisha jina kutoka jina binafsi kuwa taasisi, Nafikiri ni jambo linalowezekana kwa hivyo naomba atuachie tushauriane ili tulifuatilia vizuri ili lile lengo lilokusudiwa liweze kufanikiwa kwa ukamilifu wake.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimuhakikishie kwamba jambo hili tutalifuatilia serikalini ili kuhakikisha hii kesi inakwenda na matokeo yanaonekana na maslahi ya nchi yanalindwa. Kwa hivyo ushauri huu tunaupokea vizuri.

Kwenye suala la kumpatia ulinzi kijana wetu huyu aliyefanya kazi nzuri, ushauri huo tumeupokea na tutaufanyia kazi na kuanzia sasa tayari hizo shughuli zinafanywa ili kuhakikisha ulinzi wa kijana wetu unakuwa makini

kwa usalama wake. Tutalifuatilia kwa kina zaidi hili suala. Ahsante sana na namshukuru sana kwa hilo.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana na baada ya uhakikisho wa mambo hayo mawili hasa hili la kumlinda ndugu yetu huyu nashukuru. Sisi wengine humu ndani tumeshakufa wadudu, tumejitolea kwa hivyo huwa hatujali lolote litakalotufika. Lakini kwa watendaji wetu hawa suala la kulindiwa usalama wao wanaposimamia masuala ya haki kama haya ambayo ni nadra kwa serikali yetu. Tumeona watendaji wengi wanashindwa kufanya kazi kama hiyo, basi tuthamini kwa juhudi zake na kutoa mfano kwa wengine serikali kuwalinda inawapa moyo na inatoa muelekeo wa vipi watendaji wetu hawa.

Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, tunashukuru kwa hatua hizo na naamini kwamba zitatekelezwa hazitoishia katika Baraza tu hapa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nasema tuendelee.

Kifungu 0016	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja	379,526,000

Kifungu

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nashukuru kunipatia na mimi nafasi hii. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi na Naibu Waziri jinsi walivyoelezea mambo yao. Sasa hivi kweli wizara imepata watu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sijakubaliana kabisa na Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, kanieleza mambo, nasema kanikoroga, nisingesimama hapa, lakini Waziri wa Biashara kanikoroga.

Serikali hii hufanya mipango yake kwa kujua na kwa kupanga Sera na Mipango na Utafiti. Sasa kama hatukufanya sera, na sera ndio muongozo wa kutuongoza, hatukufanya utafiti, hatuwezi tukafika pahala tukasema tumejiunga na Umoja wa Kimataifa. Bara wamekataza makuku mabovu haya, sisi hapa kila kitu huu, huu, huu tukumbizie hapa. Tusiwe hivyo! Mimi nakubaliana kwamba kuna mambo tunaungana kwa nia safi kabisa kwa maslahi ya Zanzibar, lakini tusijaribu kusema maneno ambayo tukawavunja moyo wananchi wetu.

Suala hili Mwenyekiti, niachie nizungumze leo kinagaubaga. Hii ni Wizara ambayo ni Wizara nyeti katika serika yetu. Ni wizara ambayo ndiyo itawakomboa wananchi, kimaisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe kinachohitajika sasa hivi hapa ni hoja. Kwenye kuchangia tumeshapita sasa tunakwenda kwenye kupitisha vifungu na hoja.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, natoa hoja ndio maana nikasimama, kama sikutoa hoja nisingesimama. Mhe. Mwenyekiti, niachie nitoe hoja, kama sikufahamisha kama alivyotufahamisha Waziri wa Biashara na Mawaziri wawili hawa, na mimi natoa hoja ndio maana nikasimama hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sawa nimekubali, lakini toa hoja kwa ufupi ili ueleweke na upate majibu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mimi Mhe. Mwenyekiti, nimeletwa na wananchi hapa. Na wanaopata shida ni akina mama zaidi. Kwa hivyo mimi natetea wananchi ambao akina mama ndio waliozaa akina baba. Mhe. Mwenyekiti, sisi tuna majukumu kwa wananchi wetu. Makuku yale, nayasemea tena paja la kuku limekaa kama paja la mbuzi, serikali lazima ingejipanga mwanzo. Tusiseme kwamba tunamlinda mlaji. Sisi wenyewe ndio tuliofanya makosa, hatukutafiti, Sera hatuzitumii, hatuishauri serikali vizuri. Tungefanya mambo hayo mimi nisingekuwa mkali leo hapa, mimi sistahiki kwa sababu hii ni wizara yangu katika Kamati.

Nasema haya kwamba Mawaziri wafanye wajibu wao ipasavyo. Ili tuhakikishe wananchi wetu tunawatetea. Mimi hapa Mhe. Mwenyekiti, natetea wananchi. Naiomba Serikali Kuu initamkie hapa, sipitishi! Nataka nijue wenzetu Bara kwa nini, kwa sababu sisi tunajaza mikataba ya kimataifa tunashirikiana na Tanzania Bara. Kwa nini wenzetu wakakataza makuku mabovu yasiingie sisi tukaruhusu. Tulinde ajira ya ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti: Hoja yako ya msingi Mheshimiwa.

Mhe. Asha Bakari Makame: Nataka nihakikishiwe kwamba ajira ya ndani ya nchi inalindwa.

Mhe. Mwenyekiti: Hiyo ndiyo hoja yako ya msingi.
Mhe. Asha Bakari Makame: Nasemaje, serikali inihakikishie.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, nataka niungane na Mheshimiwa mama Asha Bakari, kwa namna ambavyo amesimama imara kuwatetea wananchi na wafugaji wetu na ndio msingi huo huo wa serikali, nia na madhumuni makubwa ni

kujitosheleza kwa uzalishaji wa aina zote ukiwemo wa kuku hapa ndani ya nchi yetu, tusingependa kabisa kuagiza vitu vyetu kutoka nje.

Nia na madhumuni tunajipanga tuzalishe ndani. Nataka niseme kabisa kwamba si ruhusa kuingiza kuku wabovu, hairuhusiwi kuingia kuku wabovu, kuku wanaoruhusiwa kuingizwa nchini ni wale ambao watatimiza vigezo vyote vinavyotakiwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. Alichosema Waziri wa Biashara alikuwa anasimamia kwamba kuku wanaoruhusiwa kuingizwa ni wale wazima wanaotimiza masharti. Vile vile tumeweka suala zima la kuongeza kodi ili ku- *discourage* uingizaji huo wa kuku kutoka nje na kutoa nafasi kwa wazalishaji wetu wa ndani.

Kwa hivyo nataka nimuhakikishie mama Asha kwamba ushauri wake tunaupokea, tutakwenda tuufanyie kazi zaidi vizuri ili kuhakikisha kwamba wananchi wetu wote hasa wazalishaji wa kuku wanapata fursa ya kuzalisha kuku zaidi. Lakini tuhakikishe kwamba na Sekta yetu ya Utalii isiporomoke na inapata mahitaji yake yanayohusika. Kwa hivyo yote haya tutayapanga vizuri, kuyawekea mikakati vizuri ili isilete taathira kwa wazalishaji wetu, na wakati huo huo tuweze kuziba pengo lile ambalo lina upungufu wa idadi ya mahitaji ya kuku nchini, na kuku wote wabovu si ruhusa kuingia ndani ya nchi na watakaofanya hivyo watachukuliwa hatua kali.

Na napenda tena nirudie na kumuunga mkono Mhe. Waziri wa Biashara pale aliposema watu wetu wa kodi wasimamie suala zima la biashara hii ya kuku, wale kuku wanaoingizwa nchini ili kodi walipishwe kwa asilimia mia moja kwa mujibu wa taratibu ya kodi iliyowekwa ili uweze kutoa tofauti ya kibei na wananchi wetu waweze kuuza kuku wao kwa vizuri zaidi.

Mhe. Asha Bakari Makame: Kwa sababu serikali kuu imetoa tamko kuku ukiwachemsha maji hayakauki maisha wewe unachemsha tu, mimi sina matatizo hapo nitakapokuwa sijapata jawabu hapakaliki.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nilipochangia suala hili mimi nasema yanaitwa peduu. Mheshimiwa na mimi nina *point* zangu ninakwenda kwenye *point*. Mheshimiwa niseme kwanza sikubaliani na kauli ya Waziri aliyekaa sasa hivi wa serikali, sikubaliani naye hata kidogo kwanza kwa sababu nina sababu zangu muhimu na sababu zangu ninazitoa. Mheshimiwa hivi karibuni kuna ndizi ambazo zimezuiliwa na Wizara hii ndio iliyosema kuwa ndizi hizi hazifai kuingizwa ndani, lakini Mhe. Mwenyekiti kuku anatoka Brazil mpaka kuingia Zanzibar ana miezi 3 ni kitu ambacho kinaingia katika friji.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe nenda kwenye hoja.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ndio ninaendelea Mheshimiwa, huwezi kupata hoja kama hukupamba hoja ndio ninaingia kwenye *point* sasa mimi nitajibu *point* moja kwa moja haiwi raha hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hatuna muda wa kupamba hapa sasa hivi twende hoja tumalize hii Wizara leo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Sawa Mheshimiwa ndio naendelea katika hoja kutoa *point* zangu. Mhe. Mwenyekiti nipe raha kwa sababu nimekula kiapo mimi kwa msahafu na Mheshimiwa unaona kitabu kimoja hiki cha *qur-an* tukufu na leo siku ya Ijumaa naomba unipe raha Mheshimiwa kisinitie dhambini hichi na nyinyi msiingie dhambini kwa kitabu hiki kikubwa albadiria hii. Naomba sana. Kwa hivyo Mheshimiwa ninasemaje, Mhe. Naibu Waziri alipotoa hoja hapo alisema neno moja ni zuri sana kwa sababu sisi hatuna mkataba lakini wenzetu kule wana mkataba.

Mheshimiwa naomba sana Mheshimiwa kwa kuwa sisi tumekuwa sisi mwenzetu ambao tunaotegemea mkataba wao haujaridhiwa katika Baraza hili, na sisi tukubaliane nao Mheshimiwa. Hawa kuku Mheshimiwa mapaja makubwa kama paja langu tusiwalete hatutaki. Mheshimiwa TASAF iliweka bilioni moja kwa makusudio ya kuwawezesha wananchi wetu wafugaji wa kuku, kwa nini tulishindwa, ina maana kumbe kulikuwa na utafiti mimi nina wasiwasi mmoja Mhe. Mwenyekiti kwa kumalizia hoja yangu ili nipate jibu, Mheshimiwa hebu tuambizane ukweli, mradi huu pengine una wakubwa humu ndani tuseme ukweli kwa lengo la kutaka kuwamaliza wananchi wa Zanzibar.. *(Makofi).*

Mheshimiwa tumeletewa unga mbovu, Mheshimiwa tumeletewa mchele mbovu, Mheshimiwa hata *insulin* tumeletewa ndio hivyo hivyo. Sasa Mhe. Waziri sikubaliani nalo hili suala mpaka sasa kwa sababu hawakuwa na hoja ya kunijibu. Naomba Mhe. Waziri atoe kauli ya kuzuia mara moja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. naomba kwanza tufuate taratibu zetu tunazokubaliana kwa mujibu wa kanuni. Mheshimiwa katika wakati huu tunapojadili suala hili la bajeti si vizuri kutoa tuhuma za wakubwa wanaoshirikiana. Tunaomba Mheshimiwa Mjumbe awataje wakubwa hao wala asione kisisi, kama wapo atupe ushahidi wa jambo hili kama wapo awataje hapa ndani.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, anayefahamu Kiswahili nilichozungumza nimesema kuwa au hebu anifahamishe Kiswahili au pengine mradi huu una viongozi, hebu nataka anielewe Kiswahili mimi nina akili yangu Mheshimiwa, wananchi wa Jimbo la Kitope wamenichagua

kwa kunijua nina akili si kusema *directly* naomba mnifahamu Mheshimiwa. Hii UNDP ndio iliyonisomesha mimi hapa kupitia Baraza la Wawakilishi mimi siku-*direct* kusema mtu *specific* mtu kuwa dokta fulani au mtu fulani anahusika na suala hilo. Nimesema au mradi huu una viongozi haya nikamateni sasa hivi hapa Mwanasheria nyanyuka unijibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hata kanuni zinakataza tuhuma huwezi kutuhumu watu wakati huna uhakika, ilikuwa ni tuhuma kwa sababu unasema au wakubwa wamo.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mimi nimesema au jamani au ni sawa sawa kusema yaumu shaka, yaumu shaka nimesema ni nani nimemuonesha hapo Mheshimiwa, na wasiwasi kitu ukisema wasiwasi Mheshimiwa hakikubaliki sasa Mwanasheria anitupe jela.

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mheshimiwa wasiwasi ndio tuhuma lakini tufanye hivi kwa kuwa muda wetu unakwenda tumpishe Mhe. Waziri ajibu ili upate ufafanuzi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mimi niko tayari anijibie suala langu tu basi Mheshimiwa aliyesimama ndio aliyesema hilo. Mimi nataka Mhe. Waziri ajibu anambie *no, stop* makuku haya hayapiti basi. Nimemaliza mimi Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti kanuni zetu zinatukataza kutuhumu, kama huna uhakika hilo jambo ni bora unyamaze kimya usiliseme, kama unalisema uwe una hakika ya kile unachokisema. Kwa hivyo Mheshimiwa hakuna Kiongozi au wakubwa wanaoshirikiana katika suala la kuleta kuku wabovu hapa nchini. Aombe radhi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Kwa kutumia kanuni na unaonesha na kifungu fulani ambacho kinaeleza hivi. Mhe. Waziri kasimama tu na kueleza hajasema kifungu gani na nini. Lakini narudia tena Mhe. Mwenyekiti sikum-*direct* kusema kama Waziri fulani ndiye anayehusika, nimesema jambo la yaumu shaka. Jamani hili neno la yaumu shaka halikuwa na makamilisho. Nimesema au, au *it means* ndio yaumu shaka hiyo Mheshimiwa Mwenyekiti tusijishuku Mheshimiwa, mimi naomba sana tumpe fursa Mheshimiwa wetu Waziri anijibu labda ninaweza nikaridhika na jibu lake mchezo ukaendelea Mheshimiwa, *well* sasa hivi tunaendelea.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kifungu 59(3) kinasema hivi "Mjumbe yoyote yule anaposema Barazani atawajibika kuwa

na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu. Na Spika au Mjumbe mwengine yoyote anaweza kumtaka Mjumbe huyu anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika. Na yeye anataka uthibitisho wa wahusika, nani wanaohusika wakubwa gani katika nchi hii wanaruhusu kuingizwa kuku wabovu?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mshimba Mhe. Waziri hicho kifungu ambacho ulikuwa unakitaka tayari ameshakizungumza na ninafikiri umekielewa vizuri. Sasa tunataka kauli kutoka kwako.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mheshimiwa hebu hiyo tafsiri aielewe vizuri na mimi ninavyozungumza vizuri. Mheshimiwa nasema tena sikumtuhumu mtu nimesema au kuna watu ambao wameshiriki au, au, *it means* au au hawa watu nani? Mhe. Mwenyekiti hebu nielewe watu wa aina gani, mimi Mheshimiwa siombi radhi kwa hili, nasema kweli kwa sababu ninajiamini ninachokisema au kwa sababu sijaenda *direct* kumsema mtu. Na hoja yangu nzito kwa nini tunashindwa Mheshimiwa kutoa hoja kusema kuwa mkataba wenzetu Bara wameshavunja na sisi watoto tuvunje mkataba ndio hoja yangu nzito hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tumebakiza muda mchache sana wa kulumbana kwenye hili ningemuomba sana Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu atusaidie kwa hili ili tumalize tuendelee.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti ninashukuru ni kweli kuwa muda wetu uliobaki ni mfupi na nilitegemea kwa mila na desturi za wanasheria kwa Mwanasheria Mkubwa pale unapoteleza angesema hapa nimeteleza. Maana kanuni inasema wazi kwamba kutuhumu inakataza, kusema jambo la kubahatisha inakataza, kusema jambo ambalo huna hakika pia unakatazwa. Yeye mwenyewe anakubali hana hakika hicho anachokisema, kwa hivyo ni vizuri Mhe. Mshimba aseme kwamba hili sina hakika ni kweli kwa mujibu wa kanuni nimekosea tuendelee. Aturuhusu tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti naona kuwa hoja yangu niliyokusudia nijibiwe haijibiwi nakwenda kwenye kanuni lakini ningemuomba sana Mheshimiwa Mwanasheria tafsiri za lugha mimi naona lazima hii kanuni kwanza irekebishwe ipite kwenye taasisi ya watu wa lugha, kwa sababu anavyofahamu yeye na ninavyofahamu mimi ni tofauti kwa mujibu wa sheria.

Niweze kusema hivi Mheshimiwa kwa kuwa muda unaenda mimi Mheshimiwa bwana....

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mshimba mimi ningeshauri kubali kwamba hili sheria inakukataza kufanya hivi kubali, kubali hivyo kanuni zinakataza kutoa tuhuma kubali hilo na kauli yako ilikuwa inaelekea huko sasa sisi tunataka kuendelea. Kubali hilo tu ili tuendelee Waziri atupe majibu yako.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti mimi ninafikiria vipi labda sijasikia vizuri hebu naomba Mhe. Mwanasheria nisomee tena hicho kifungu nikusikie vizuri.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mshimba haina haja mimi niko kwenye Kiti sasa nasemaje haina haja tunaendelea, muda hautoshi inabidi tumalize hii Wizara tunaendelea tunataka majibu kutoka kwa Waziri.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Basi Mheshimiwa acha tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Kwanza Mhe. Mshimba ufute kauli yako.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti nimeshasema tuendelee. Sasa hiyo tafsiri za mwengine.

Mhe. Mwenyekiti: Ni tofauti Mhe. Mshimba tusianze malumbano, futa kauli tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti nimeshafuta kauli yangu tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti na mimi ninakushukuru kunipa nafasi hii nikazungumza machache katika ufafanuzi ambao uliotolewa. Mhe. Mwenyekiti kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, nilipokuwa nikichangia nilichangia kwa maandishi na nilipeleka hoja yangu moja tu kwa Mhe. Waziri, lakini alipokuwa akitoa ufafauzi nimepata somo la ziada kwamba kumbe ukimkuta samaki ametulia anakuwa ni mjamzito sasa hilo kidogo nimepata faida. Lakini hoja yangu Mhe. Mwenyekiti wenzangu walizungumzia kuku wabovu, mimi sizungumzii kuku wabovu, mimi hoja yangu ninakuja kwamba serikali inahamasisha wananchi kufuga na wakiwemo wafugaji wa kuku. Mhe. Mwenyekiti mimi niliwahi kuwa Waziri katika Afisi ya Waziri Kiongozi na nilipita Unguja na Pemba kuhamasisha wananchi hasa kinamama kufuga kuku, na miongoni mwa watu waliohamasika kufuga kuku ni wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura, baada ya serikali kuruhusu kuku wa peduu kuingia nchini, Mheshimiwa kinamama hawa wote miradi yao imekufa.

Sasa nimesikia sana hoja za Waheshimiwa mawaziri kwamba tumeridhia mikataba ya biashara *WTO*, walioridhia mikataba ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini Waziri Mateo David ambaye ni Waziri anayeshughulikia masuala ya mifugo yeye amepiga marufuku kuingizwa kuku Tanzanzia Bara leo inakuwaje sisi kuingizwa kuku kuua ajira ya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti hoja yangu nataka serikali itoe tamko la kupiga marufuku uingizwaji wa kuku wa peduu ili wananchi wetu waendelee kupata ajira ya kufuga kuku Zanzibar. Nataka maelezo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa muda tuliokuwa tumekusudia kuongeza sidhani kama utatosha tukiingia katika hayo malumbano, tumemaliza tumeingia sasa robo saa iliyobakia tunapitisha mafungu kwa jumla ili tumalize leo Wizara hii. Mhe. Hamza naomba ukae ili tunapata jibu hapa kwa Waziri, jibu lako atatoa Waziri tukimaliza tunapitisha mafungu kwa jumla. Sijazuia nimesema Waziri ajibu baada ya majibu ya waziri tunaingia kwenye mafungu ya jumla ndivyo nilivyosema nakariri kauli yangu. Waheshimiwa tumekubaliana hapa mmepitisha wenyewe.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti sijui kama kanuni zetu zinaturuhusu kuendelea na mafungu bila ya kuyajadili sina uhakika huo. Sasa kama kanuni zetu zinaturuhusu kuendelea na mafungu bila ya kujadili kama utaratibu wetu tuliouzoea nilikuwa nataka maelezo. Mhe. Mwenyekiti hoja zetu ni za msingi tunahitaji maelezo ya kutosha kabisa. Mimi nashauri bora tuakhirishe Baraza twende tukasali turudi tuje tuendelee na utaratibu mpaka tumalize fungu. (*Makofi*). Mhe. Mwenyekiti hilo hakuna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tulipoomba Mhe. Waziri aliomba kuweka kanuni kando na tulikubali haya yote ili kwamba ukifika muda tunapitisha kwa mafungu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Kwa kuwa suala la uingizaji wa kuku kutoka nje limeleta mjadala mkubwa katika Baraza lako hili, na sote tunajua umuhimu wa wafugaji wetu wa ndani. Lakini tunajua umuhimu pia wa lile pengo la idadi ya mahitaji ya nyama ya kuku nchini. Kwa hivyo tukitoa tangazo la kupiga marufuku moja kwa moja bila ya kufanya tathmini ya kina tukajua na athari zake, kwa sababu kama alivyosema Waziri wa Biashara, bado yapo mapungufu kutokana na idadi inayozalishwa ndani na idadi inayohitajika upo upungufu.

Kwa hivyo kwa njia moja au nyengine tunahitaji kuku kutoka nje, ikiwa kuku tunawahitaji ni wale kuku wenye afya njema, wenye maslahi ya wananchi kwa maana ya afya zao, haturuhusu kuku wa aina yoyote yule mbovu. Kwa hivyo nilikuwa nawaomba Waheshimiwa mtukubalie mtuachie jambo hili

tulitafakari kwa kina, kwa sababu kutoa tangazo la kupiga marufuku na pengine ikatokezea upungufu mkubwa mahitaji ya nyama ya kuku ndani ya nchi yetu ni athari kwetu sote na ni athari pia kwa sekta ya utalii.

Na kama alivyosema Waziri wa Biashara yanaweza kujitokeza malumbano ya kitaifa kutokana na masuala mazima haya ya biashara na *WTO*. Kwa hivyo nilikuwa nawaombeni tu Waheshimiwa mtuachie hili jambo tukalifanyie kazi, tusilifanyie haraka katika kuliamua kwake ili tupime kwa kina athari na mafanikio yake, nia yetu sote na nia ya serikali kuona tunazalisha kila kitu chetu hapa ndani. Tunataka wafugaji wetu wazalishe wenyewe kuku wa kutosha, ng'ombe wa kutosha, chakula cha kutosha, na ndio maana serikali inaweka bajeti maalum kwa ajili ya kusaidia wakulima wetu ili uzalishaji nchini uongezeke.

Kwa hivyo tunazungumza lugha moja, tunachokisema tusije tukatoa athari ya kutokea mapungufu makubwa halafu tukasumbua wananchi, tukasumbua na sekta ya utalii ambayo ndio sekta mama ya uchumi wa nchi yetu. Sasa tunawaombeni Waheshimiwa mtupe muda tulishughulikie jambo hili, tunakubali kupokea ushauri wenu, tunaujua umuhimu wa wafugaji wetu, tunajua umuhimu wa wazalishaji wa ndani. Naomba Waheshimiwa tukubaliane na hili tukalifanyie kazi. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hivi kwamba suala la kuzuia wala hatutokuwa na tatizo katika suala la *WTO*. Kama nilivyosema Tanzania Bara wao ndio walioridhia Bunge la Jamhuri ya Muungano lakini wao wamezuia mbona hakujatokea mgogoro wa *WTO* na Tanzania Bara? Sasa leo inakuwaje kwa upande wa Zanzibar. Lakini kubwa zaidi Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hivi mimi nimetembelea *incubator* karibu tano hapa Zanzibar, ikiwemo Fuoni, sitaki kuzitaja sehemu zote, Mheshimiwa wananchi wamehamasika, na mimi kama nilivyosema mimi nilifanya ziara kipindi hicho cha nyuma Mheshimiwa wananchi wameitikia, kuna *incubator* karibu tano kubwa wanazalisha vifaranga 3000 kwa siku, leo vifaranga vile wanasafirisha Tanzania Bara kwa sababu Zanzibar soko hakuna. Na kwa sababu wanakuwa kutokana na bei ya hawa kuku wa peduu, wananchi wetu hawawezi wakauza na wenzetu kule Brazil wanafidia wana-*subsidize* kuku wanapoumwa serikali inafidia, hapa kuku akiumwa anaumia na mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti suala tukizuia hakuna tatizo lolote kwani yalipozuka mafua ya ndege si walizuia ndege wote na wanyama wote kusafirishwa, nani aliyelalamika? Mheshimiwa tumefunga soko tumefunga ajira kubwa kwa wazanzibari, juzi Mhe. Mwenyekiti wewe ndiye uliyekwenda kutoa pesa milioni 13 ukawapa kinamama kwa ajili ya miradi ya vikoba. Sasa wao vikoba wanakwenda kufuga kuku watamuuzia nani? Utatoa

milioni 13 utakwenda kutoa nyengine. Mhe. Mwenyekiti katika suala hili mimi ninafikiri Mheshimiwa wala usione kama labda kama unafanyia *game*. *We are serious* katika hili, hatukubali mradi wa kuku wa peduu kuingizwa hapa nchini.

Mhe. Spika, tunataka kufungua ajira ya watu wetu Mhe. Kikwete alitangaza ajira elfu kumi sijui elfu kumi na moja. Dr. Shein katangaza tutasaidia ajira kwa vijana na akinamama, leo tumezuia ajira zaidi ya watu 5000 kwa biashara ya watu 20. Mimi situhumu watu lakini biashara ya watu 20 imezuia ajira ya watu zaidi 5000 tunakwenda wapi? Sisi ndio tunaopitisha bajeti ya serikali ndio tunaotetea maslahi ya wananchi. Mhe. Mwenyekiti mimi naomba sijakubaliana na yote yaliyozungumzwa, suala kama wananchi watafunguliwa. Sasa unajua zamani ilikuwa vifaranga vinatoka Afrika ya Kusini ndio maana kuku walikuwa hawatoshelezi. Sasa hivi wananchi wetu wamehamasika vifaranga wanatotoa hapa hapa.

Mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti serikali isione tabu tulinde ajira ya wananchi wa ndani tuzuie kuku wa peduu tuendelee na bajeti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti anayoyasema Mhe. Hamza ndio yale niliyoyasema, serikali ingependa sana kuona tunatoshelezeka na uzalishaji wa ndani, na ndio nia yetu na ndio maana tumehamasisha wazalishaji wa ndani waweze kuzalisha. Tatizo lililojitokeza lazima tukubali ukweli. Takwimu zinaonesha yapo mapungufu tunahitaji kulijaza hilo pengo la mapungufu hayo.

Kwa hivyo mimi nishauri kitu kimoja kwamba tukae sisi na wadau na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wataalam wetu na wafugaji tulizungumze hili kwa upana wake tupate maamuzi muafaka. Tusije kutoa maamuzi kwa pupa tukaja tukaleta athari ndani ya nchi yetu, kukatokea mapungufu makubwa ya nyama ya kuku kitu ambacho kitawaathiri wananchi, kikaathiri sekta ya utalii, kitatuathiri sote. Lakini nia na madhumuni bado tuna nia kubwa ya wananchi wetu hawa waweze kuzalisha vizuri kwa namna yoyote ile, tungependa wafanye hivyo na ndio maana tunaelewa kwamba ipo *subsidise* hasa huko Brazil, na ndio maana tukaongeza kodi, msingi wetu wa kuongeza kodi tunawafanya wale kuku kutoka nje wawe na bei kubwa waishinde bei ya ndani ili kuku wetu wa ndani waweze kuuzwa, na kwa vyovyote vile kuku wa kienyeji ni kuku wazuri wenye nyama nzuri, kwa vyovyote vile hawawezi kukosa soko la ndani.

Kwa msingi huo mimi nakubaliana kabisa kwamba tukubaliane tukae pamoja wahusika sote tukalifanyie kazi hili jambo hatuna nia ya kuwasumbua wananchi wetu, nia yetu ni kufanya jambo lenye maslahi yetu sote isije

ikatuathiri. Kwa hivyo sote tuna imani ya wananchi, sote tuna imani ya wafugaji, sote ni wazalishaji wa pamoja lakini pia nitanabahishe kwamba leo ni Ijumaa na wakati umefika Mhe. Mwenyekiti ili tusije tukachelewa zaidi naomba muongozo wako. Ahsante sana.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe ule muda ambao tulikubaliana kwamba mpaka kufikia saa sita na nusu basi tutaliakhirisha Baraza hili, lakini kutokana na hoja ambazo zimeletwa na Wajumbe mbali mbali hapa nimeona ipo haja ya serikali kwenda na kuzingatia hoja za Wajumbe na kuja Jumatatu kwa ajili ya kuleta maamuzi.

Waheshimiwa ninawashukuru sana leo kwa utulivu wenu, naakhirisha kikao hadi Jumatatu tarehe 29/07/2013 saa 3.00 asubuhi.

(Saa 6.30 mchana Baraza liliakhirishwa hadi

tarehe 29/07/2013 saa 3.00 asubuhi)